Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

لا إله إلا الله محمد رسول الله

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Mwenyezi Mungu wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kupita kiasi bila kujua. Hivyo Tumewapambia kila watu vitendo vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye Atawaambia waliyokuwa wakitenda. (6:109)

JUZU 74 No. 183 | SHWL./DH.QA'DA 1436 AH | AGOSTI 2015 | ZAHOOR 1394 HS | BEI TSH. 500/=

Homa ya uchaguzi 2015 Mwenyezi Mungu Atuponye



Mh. John Joseph Pombe Magufuli, akinadi sera za Chama chake mbele ya wapiga kura katika moja ya mikutano ya kampeni.



Mh. Edward Ngoyai Lowassa, akinadi sera za Chama chake mbele ya wapiga kura katika moja ya mikutano ya kampeni.

Na Mahmood Hamsin Mubiru, Dar es Salaam

Mashabiki wa masumbwi watakumbuka mnyukano wa karne baina ya George Forman na Muhammad Ali katika Jamhuri ya Demokrasia ya Congo mwaka 1975. Tumepata fursa ya mnyukano mwingine safari hii katika uwanja wa siasa za Tanzania kati ya Mwalimu John Joseph Pombe Magufuli wa Chama cha Mapinduzi na Mwalimu Edward Ngoyai Lowassa anayepeperusha bendera ya UKAWA kwa kupitia chama cha Demokrasia na Maendeleo - CHADEMA.

Ni mchuano katika maana kamili ya neno hilo. Wote wawili wanawakilisha vyama vyenye nguvu na wafuasi wengi nchini. Wawili hao sio wageni katika kumbi za siasa na madaraka. Ni wasemaji wazuri. Wachapa kazi na wafuatiliaji. Ni wasomi wa haja, na wote wakiwa na mapenzi ya watu wa hali ya chini. Wote wamesomea ualimu ingawaje mmoja aliwahi kufundisha na mmoja hakuwahi. Mmoja anakumbukwa kwa kunasibishwa na shule za kata wakati mwingine anasifika sio tu katika ujenzi wa barabara bali hata kukumbuka majina ya barabara zenyewe na madaraja, pamoja na urefu wa barabara hizo.

Kule wanakotoka wana mizizi iliyoenda chini na hutokea mara nyingi kupitishwa bila kupingwa na huko hakuna mwenye uwezo wa kuwatikisa.

Wote wawili wameleta msituko, kwa upande wa Magufuli alikuwa wa mwisho mwisho kutangaza nia na alipita sehemu zote bila mbwembwe za aina yoyote. Kwa upande wa Edward Ngoyai Lowassa msituko ni ule alipokiacha chama chake ambacho amekitumikia kwa miaka mingi, lakini msituko uliongezeka zaidi alipojiunga na kambi ya upinzani na kuendeleza kile

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

MAPENZI YA NCHI

Unaposikia shairi la Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote, hapana shaka moyo unasisimka, unapata furaha kubwa na wale wenye machozi yaliyo karibu kuna uwezekano yakadondoka. Nchi ni mama na watu huuliza siku zote 'nani kama mama'!

Kwa bahati mbaya nchi yetu imefanikiwa kuwa na vitu vingi ambavyo vinaweza kutusukuma kwenda mbele. Jambo moja tu tumekosa nalo ni mapenzi, jazba na mahaba kwa nchi yetu. Ni wangapi kati yetu tunapoiona bendera ya nchi yetu tunasisimka na kimoyomoyo kuapa kuilinda. Ni wangapi maneno ya ujumbe wa wimbo wa taifa letu yana maana 'Mungu Ibariki Tanzania' je ni kweli katika ibada zetu tunakumbuka kuiombea nchi yetu?

Lakini ipo mifano ya watu waliokuwa na mahangaiko makubwa na kwa dua za vilio walikuwa wakiililia nchi hii na matokeo yake ni amani ambapo sote tunaionea furaha.

Kuna haja ya kuamsha mapenzi ya taifa katika nyoyo za watanzania. Allah Ametupatia kila kitu, rasilimali, utulivu, lugha moja. Kuwa na lugha moja peke yake ni neema kubwa. Jamaa kutoka India alipokuja nchini na akakuta tunazungumza lugha moja aliinua mikono na kushukuru, kwani kwao India wana lugha kubwa 17 hebu niambie lugha 17! Machozi yalimtiririka alipoona ardhi kubwa yenye rutuba ikiwa tupu. Hakuamini alichokiona. Kweli penye miti hapana wajenzi. Lakini haya yote kwa nini yanatokea? Tumepoteza kabisa uzalendo na mapenzi ya taifa letu. Kwa nini kila mtu anajifikiria yeye binafsi na sio taifa? Taifa gani limewahi kuendelea bila ya watu wa taifa hilo kuwa na mapenzi na nchi yao?

Na mapenzi sio matangazo. Sio kujigamba. Mapenzi kimsingi ni vitendo. Ukiingia katika mikataba yenye kudhuru wananchi hayo ni mapenzi ya aina gani? Ukitaka chochote kwa kazi uliyopewa na umma, hayo si mapenzi! Ukipita unawakoga wengine kwa mali uliyokusanya kwa njia zisizoeleweka hayo si mapenzi ni kibri!.

Mapenzi ni utumishi. Mapenzi ni kutimiza wajibu. Ukiwa peke yako na umezungukwa na watu, dhamira yako itakusuta, haya ndiyo mapenzi ambayo tumeyakosa. Nchi yenye rasilimali, amani, lugha moja, inakuwaje kushindwa kupambana na umasikini, maradhi na ujinga.

Hata hivyo hatuwezi kubeza asilani jitihada iliyofanywa lakini basi jitihada hiyo isitufanye tubweteke. Tuendelee kupambana. Tuipende nchi yetu, na daima tutawaliwe na kauli iliyotolewa na aliyewahi kuwa raisi wa Marekani John Kennedy aliyewaambia Wamarekani 'Usiulize nchi yako itakufanyia nini, bali uliza wewe utaifanyia nini nchi yako'. Nchi hii ina fursa nyingi. Nchi hii ina mahitaji mengi. Nchi hii milango iko wazi.

Linalotakiwa kwa sasa ni kila mtu kutoa jasho kuleta maendeleo nchini.

Inawezekana timiza wajibu wako.

Mungu ibariki Tanzania.

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Omar Ali Mnungu
Wajumbe:
1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Homa ya uchaguzi 2015

Kutoka uk. 1

kitu anachokiita "Mabadiliko nje ya CCM".

Wote wawili wameanzisha ufalme huko wanakotoka, wamekuwa Wabunge kwa miaka mingi ni muhali kuzungumzia siasa za Chato bila kumtaja Magufuli kama ilivyo vigumu kuzungumzia Monduli nje ya Lowassa.

Historia imewaleta pamoja miamba hawa wawili wa siasa, nia ni ile ile kushindana katika kuwatumikia wananchi. Maelezo yao, jana yao, vitasaidia kwa wananchi kufanya uamuzi ambao unakuja mara moja katika miaka mitano. Si wakati wa kucheza. Ni wakati wa kuamua. Na waswahili kama wasemavyo, kusuka au kunyoa.

Hata hivyo tukumbuke kwamba binadamu anaweza kwenda kwa kiasi fulani. Ni kiasi fulani. Anachohitaji katika vyote ni msaada wa Allah Anayejua mambo ya ghaibu. Yeye pekee ndiye anayeweza kutusaidia kufanya uamuzi wa busara. Tukiachiwa peke yetu uwezo wa kupotea ni mkubwa kwani huenda tukapenda kitu kumbe kuna shari ndani yake na tukachukia kitu kumbe kina kheri ndani yake. Hapo tunahitaji msaada wa Allah ili kutuongoza kwenye njia iliyonyooka. Bila shaka kupiga kura ya kuwachagua viongozi wa kitaifa ni haki ya msingi kama sio faradhi kwa Muislam.

Hadhrat Mirza Tahir Ahmad, Khalifatul Masih IV r.h, ana haya ya kutukumbusha katika kitabu chake ***Islam's Response to Contemporary Issues*** (uk. 230):
Dhana ya Kiislam ya demokrasia ina nguzo mbili za msingi.

1. Shughuli ya demokrasia ya uchaguzi inapaswa iwe kwa uaminifu sana. Islam inatufundisha kwamba daima ikumbukwe wakati wa kutumia haki ya kura kwamba Mwenyezi Mungu Anatuona. Basi tunavyowajibika uamuzi wetu vile vile tunawajibika mbele ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo kura apewe yule ambaye anaweza kutimiza jukumu lile la kitaifa bali mwenyewe pia awe mwaminifu. Katika fundisho hili jambo hili pia limefichika kwamba watu wote walio na haki ya kupiga kura lazima watumie haki yao isipokuwa washindwe na hali au kiwepo kipingamizi chochote njiani cha kutumia haki hiyo.

2. Nguzo ya pili ya demokrasi ya Kiislam ni hii kwamba wakati wa maamuzi uadilifu kamili ufuatwe. Serikali zinapaswa kufuata kanuni ya uadilifu kamili. Uadilifu usiachwe katika hali yoyote.

Hivyo ni lazima tumuelekee Mwenyezi Mungu kwa dhati kabisa na kumuomba kwa uaminifu wetu wote kwamba sio tu uchaguzi uende kwa amani na salama bali pia atupe busara ya kutumia kura yetu kwa uaminifu, lakini hatima ya yote atujaalie yule Kiongozi ambaye atakuwa na kheri zaidi kwa ajili ya mustkabali wa maendeleo ya taifa letu. Ushabiki na mihemuko ya kisiasa isitufanye kusahau maombi haya.

Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alitufundisha kwenye dua ya Sala ya Isitikhara kwamba hata kama vitu viwili vinavyokupendeza vipo mbele yako, na ukapewa nafasi ya kuchagua kimoja basi bado unatakiwa umuombe Mwenyezi Mungu Akujaalie kile kilicho na kheri zaidi kwa ajili ya dini yako na dunia yako pia.
Hivyo basi, sote tuombe.

1. Ya Ilahi Ya Karima, vyote Kwako hurukuu
   Ni kubwa yako Adhama, Upweke Wako Ukuu
   Twakuomba kwa heshima, mikono ikiwa juu
   Uchaguzi mwaka huu, Mola Uupe salama.

2. Mola Uupe salama, Uchaguzi mwaka huu
   Nyoyo zetu zatetema, kila mtu roho juu
   Uchao yapanda homa, ya uchaguzi mkuu
   Uchaguzi mwaka huu, Mola upite salama.

3. Mola upite salama, Uchaguzi mwaka huu
   Uende kwa mwendo mwema, si kuzidiana dau
   Sote tupe nia njema, milima na vichuguu
   Uchaguzi mwaka huu, Mola ujaze salama.

4. Mola ujaze salama, Uchaguzi mwaka huu
   Uokoe huu umma, kufanyiana dharau
   Uuwezeshe kusema, kwa adabu na nahau
   Uchaguzi mwaka huu, Mola uwe wa salama.

5. Mola uwe wa salama, Uchaguzi mwaka huu
   Sote tujaze hekima, tusome ile nukuu
   Iliyotukia nyuma, kwa wana wa Mau Mau
   Uchaguzi mwaka huu, umalizike salama.

6. Umalizike salama, Uchaguzi mwaka huu
   Sikiangalie chama, chungwa au zambarau
   Pitisha zako karama, tupe chenye unafuu
   Uchaguzi mwaka huu, Mola bariki salama.

7. Mola bariki salama, Uchaguzi mwaka huu
   Anayeulia njama, Mola mbeue beu
   Na apangaye dhuluma, Mlipizie makuu
   Uchaguzi mwaka huu, Uugubike salama.

8. Uugubike salama, Uchaguzi mwaka huu
   Utukinge na zahama, ya kuvunjana miguu
   Hurumia kinamama, watoto na wajukuu
   Uchaguzi mwaka huu, naitawale salama.

9. Naitawale salama, Uchaguzi mwaka huu
   Tusije pigana vyuma, tukitoana na ngeu
   Na maji yanayouma, ja moshi wa vitunguu
   Uchaguzi mwaka huu, Mola twaomba salama.

10. Mola twaomba salama, Uchaguzi mwaka huu
    Kwa taifa lote zima, ije iwe sikukuu
    Utupe zako neema, tung'ae kama majuu
    Uchaguzi mwaka huu, Mola shindisha salama.

(Shairi na A. M. Ame)

Mafundisho yaliyo Bora kabisa

Kutoka Maandishi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Hadhrat Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa a.s. anasema:

Jueni kuwa kukiri kwa ulimi tu si kitu mpaka kufuatane pamoja na vitendo kwa nia ya moyo wote. Basi mwenye kutenda vitendo sawasawa na mafundisho yangu anaingia katika nyumba yangu iliyoahidiwa na maneno ya Mungu; "Inniy uhaafidhu kulla man fi-ddari" – Mimi nitamlinda kila aliyomo katika boma la nyumba yako. Isifahamiwe hapa kwamba waliyomo katika nyumba yangu, wao ndio wakaao peke yao katika nyumba yangu ya matofali na udongo; la, bali na wale pia wanaonifuata kwa kweli vile vile wamo katika nyumba yangu ya rohoni. Mambo yawapasayo kufuata ni haya:-
Wakiri kwa yakini kuwa wana Mungu Mmoja, Mwenye Enzi, Aliye imara na Mwumbaji wa kila kitu, ambaye katika sifa zake ni tangu na dawamu wala hazibadili. Hakuzaliwa wala hakuzaa. Naye ameepukana na kuumwa na kuwambwa msalabani na kufa. Tena Yu karibu juu ya umbali wake, na Yu mbali juu ya ukaribu wake. Ijapokuwa ni Mmoja tu lakini namna za maonyesho yake ni mbalimbali.

Yanapotokea mabadiliko mageni kwa mwanadamu ndipo Mwenyezi Mungu pia anakuwa kwa ajili yake mpya, na anamtendea mema kwa maonyesho yake mapya. Na mtu anaona kwa Mungu mabadiliko vile vile kwa kiasi cha kubadilika kwake. Lakini si muradi wake kuwa yanatokea mabadiliko katika Mwenyezi Mungu; la, bali Yeye tangu kale dhati yake haibadiliki naye yu Mkamilifu kabisa. Lakini wakati anapobadilika mtu kwenye kheri, Mwenyezi Mungu pia anajidhihirisha kwake kwa maonyesho mapya. Na mwanadamu anapoendelea kwenye wema zaidi Mwenyezi Mungu pia humzidishia kumwonyesha maonyesho yake ya Kudra. Mwenyezi Mungu huonyesha uwezo ulio kinyume cha desturi yake ya siku zote yanapoonekana mabadiliko makuu katika mwanadamu kinyume cha desturi yake ya siku zote. Na huu ndio msingi wa ishara na uwezo wake wa namna hii. Mungu huyu ni sharti ya Silsila yetu.

Basi mwaminini na mtangulizeni juu ya mioyo yenu, na juu ya raha yenu, na juu ya kufungamana kwenu kokote. Na onyesheni katika njia yake ukweli na kutekeleza kwa vitendo vyenu na ushujaa. Watu wa dunia hawamtangulizi Mungu juu ya jamaa zao na vitu vyao; lakini ninyi mtangulizeni Mungu ili muandikwe mbinguni Jamaa Yake. Kuonyesha ishara za rehema ni desturi ya Mungu toka zamani. Lakini ninyi hamtapata sehemu yenu katika desturi yake hii ila mpaka isibakie umbali baina yenu na Yeye, na kuwa radhi yenu ni radhi Yake, na kupenda kwenu ni kupenda Kwake. Na vichwa vyenu kila wakati na kila hali ya ustawi na kukosa viwe juu ya kizingiti chake, ili Mungu Atende Atakavyo. Kama ninyi mkifanya hivi atadhihiri kwenu Mungu yule aliyeficha Aliyefi uso wake toka zamani. Je! Yuko mmoja wenu mwenye kutenda hivi na awe mwombaji wa radhi yake wala asikasirikie hukumu na kadri yake? Basi baada ya kuona msiba endeleeni mbele kwani hii ni njia ya kukua kwenu. Na kwa kutangaza Umoja Wake duniani jitahidini kwa uwezo wenu wote.

Na rehemuni watu wake wala msiwadhulumu kwa ulimi au kwa njia ya mikono au kwa njia nyingineyo; na jitahidini kuwafanyia watu kheri. Wala msijivune kwa yeyote ijapokuwa ni watu wa chini yenu, wala msitukanane na yeyote hata akikutukaneni, na kuweni wanyonge na wapole na wenye nia nzuri na watakieni wema viumbe ili mkubaliwe.

Ni wengi wanaodhihirisha upole, lakini undani wao ni kama mbwa mwitu, ni wengi walio safi juu lakini ndani yao ni kama nyoka, basi jilindeni hamtokubaliwa na Mungu ikiwa njema ya ndani si sawa. Wakubwa wawarehemu wadogo wala wasiwafedheheshe. Na baada ya kuwa matajiri watumikieni maskini wala msitakabali juu yao kwa kujipenda. Jiepusheni na njia za maangamio, mwogopeni Mungu siku zote, na mcheni wala msiabudu kiumbe, na jitupeni kwa Mola wenu. Na chukieni dunia siku zote, na kuweni wa Mungu na ishini kwa ajili yake tu. Na kirihini kwa ajili ya radhi yake kila ubaya na dhambi kwa sababu Yeye ni Mtukufu. Inafaa kila asubuhi ishuhudie kuwa mmelala usiku kwa kumuogopa Mungu na kila usiku ushuhudie kuwa ninyi mmeshinda mchana kwa kumcha Mungu.

Msiogope laana ya dunia kwani hiyo inapotea mara moja kama moshi, wala haiwezi kubadilisha mchana uwe usiku. Bali ogopeni laana ya Mungu inayoteremka mbinguni na kuangamiza kila inayemteremkia katika dunia na akhera. Ninyi hamuwezi kujilinda nafsi zenu kwa kujionesha; sababu Mungu ambaye ni Mungu Anaona hata kilicho chini mtu. Je, mnaweza kumdanganya? Hapana! Basi juu yenu nyookeni, na jitakaseni, na jikuzeni , na tiini. Sikilizeni! Kikibaki kwenu chembe cha giza, basi hicho kitapoteza nuru yenu yote. Na ikiwa katika ubavu wenu wowote kuna kiburi au majisifu au kujipendelea au uvivu, basi ninyi si kitu kinachopasa kukubaliwa. Jihadharini na kujidanganya kwa hayo kidogo mliyo nayo na kufahamu kuwa mmefanya vilivyo vya lazima kuvifanya. Kwani Mungu Anataka yatokee mabadiliko makuu katika nafsi zenu. Na anawatakieni kifo kimoja ambacho baadae Awahuisheni.

Fanyeni suluhu upesi ninyi kwa ninyi na sameheni makosa ya ndugu zenu, kwani ni mtu wa shari asiyekuwa radhi kufanya suluhu na ndugu yake; yeye atakatwa kwa sababu ya kuachanisha watu. Acheni kabisa matamanio yenu kwa yeyote na acheni hasira zenu mlizo nazo. Nyenyekeeni kama muongo anavyonyenyekea ijapokuwa ninyi ni wakweli, ili mghofiriwe. Na wacheni unene wa mioyo kwani mlango mlikoitwa ndani yake hawezi kuingia aliyekuwa mnene kwa sababu ya makosa yake. Bahati mbaya namna gani kwa mtu asiyeamini maneno yaliyotoka kinywani mwa Mungu nami nimeyabainisha!

Mkitaka Mwenyezi Mungu Awe radhi juu yenu mbinguni, basi kuweni kama ndugu wawili waliozaliwa katika tumbo moja. Mbora wenu ni yule mwenye kusamehe sana makosa ya nduguze, na mwenye bahati mbaya ni yule mshupavu asiyesamehe; basi huyu hana ufungamano nami. Siku zote ogopeni laana ya Mungu, kwani Yeye ni Mtukufu tena mwenye Ari. Muovu hawezi kupata ukaribu kwa Mungu. Mwenye kiburi hawezi kumkaribia. Mdhalimu hawezi kumkaribia. Haini hawezi kumkaribia. Na kila asiye na ghera kwa jina lake hawezi kumkaribia, na wale wanaoangukia dunia kama mbwa na sisimizi na mbesi na wanafurahia dunia hawawezi kumkaribia. Kila jicho baya liko mbali naye, na kila moyo mchafu hauna habari naye. Atakayekuwa katika moto kwa ajili ya Mungu ataokolewa katika moto. Mwenye kulia kwa sababu ya Mungu atakuja kucheka. Na mwenye kuacha dunia atakutana Naye. Kuweni wapenzi wa Mungu kwa ukweli wa mioyo yenu, na kwa shauku sana, na kwa hamu nyingi ili Mungu pia Awe mpenzi wenu. Rehemuni walio chini yenu na wake zenu na walio maskini katika ndugu zenu, nanyi mtarehemiwa mbinguni vilevile. Kuweni wa Mungu ki kwelikweli Naye Atakuwa wa kwenu. Dunia ni mahali pa maelfu ya mabalaa; pia Tauni ni moja kati ya hayo, basi mshikeni Mwenyezi Mungu sawasawa ili Yeye Ayatenge mbali mabalaa haya. Halitokei balaa lolote ardhini mpaka kwa amri yake ya mbinguni. Wala balaa haliondoki mpaka iteremke rehema kutoka mbinguni. Kwa hivyo, akili zenu ziwe katika kukamata shina wala siyo matawi. Hamkukatazwa kutumia dawa, bali mmekatazwa kutawakali juu ya dawa. Na mwishoni yatatokea anayotaka Mwenyezi Mungu. Lakini kama mmoja wapo anaweza kushika jambo la kutawakali ni bora kuliko mambo yote.

Na mafundisho mengine yaliyo wajibu kwenu ni kuwa msiache Qur'ani Tukufu ovyo, kwani katika Qur'ani tu umo uzima wenu. Watakaoiheshimu watapata heshima mbinguni. Na watakaotanguliza Qur'ani Tukufu kuliko hadithi zote na maneno yote, wao watatangulizwa mbinguni. Sikilizeni! Na sasa hapana kitabu chochote kitakachoweza kuongoza mwanadamu juu ya ardhi ila Qur'ani Tukufu. Na hapana Mtume wala Muombezi mwingine wa mwanadamu ila Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kwa hiyo jitahidini mumpende kwa mapenzi kweli kweli Mtume huyu, Mtume wa heshima na utukufu. Na wala msimuheshimu mtu yeyote kuliko yeye ili muandikwe mbinguni pamoja na waliyookoka. Na jueni kuwa kuokoka si kitu kinachoonekana baada ya kufariki; bali kuokoka hasa ni kule kunakoonesha nuru yake hapa duniani.

Ni nani aliyeokolewa? Aliyeokolewa ni yule mwenye yakini kuwa Mwenyezi Mungu kweli yupo na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ni muombezi katikati ya Mungu na viumbe vyote. Na kuwa hapana Nabii yeyote aliye sawasawa na Mtume Muhammad, amani ya Mungu juu yake; na kuwa hapana kitabu chochote sawa na Qur'ani Tukufu chini ya mbingu. Na Mungu Hakupenda kwa yeyote awe mzima wa milele ila kwa Mtume huyu Mtukufu aliye ni mzima wa milele. Yaani Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kumuweka mzima wa milele amefungua chemchem ya sheria yake na mibaraka ya utukufu wake kuendelea mpaka siku ya Kiyama. Na mwisho kwa baraka ya utukufu wake amemtuma duniani Almasih-il-Mau'ud (Masihi Aliyeahidiwa), ambaye kuja kwake kulikuwa ni lazima kwa kukamilisha jengo la dini ya Kiislam. Maana ilikuwa ni lazima kwamba dunia hii isiishe mpaka aje masihi mmoja aliye kwa asili ya rohoni mfano wa Nabii Isa (as), katika umati wa Muhammad, amani ya Mungu juu yake, kama ulivyopewa umati wa Musa (as).

Na aya hii ya Qur'ani Tukufu; 'Ihdiinassiratal mustaqiym siratalladhiyna an'amta' alaihim' – Utuongoze katika njia iliyonyooka, njia ya wale uliyopa neema, inadhihirisha jambo hili. Na Musa (as) alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa zamani; na Muhammad, amani ya Mungu juu yake alipata mambo yaliyopotezwa na watu wa Nabii Musa (as). Na Silsila ya Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ilishika pahala pa Silsila ya Mussa (as). Lakini Silsila ya Muhammad, amani ya Mungu juu yake, ilizidi kuwa na fadhila nyingi kuliko Silsila ya Musa (as). Mfano wa Musa, (Muhammad amani ya Mungu juu yake) ni bora kuliko Musa; na mfano wa Nabii Isa, (Seyidna Ahmad as) ni bora kuliko Nabii Isa (as). Na yule Masihi Aliyeahidiwa si kwamba yeye alitumwa katika karne ya kumi na nne baada ya Mtume, amani ya Mungu juu yake kama alivyotumwa Isa bin Mariamu katika karne ya kumi na nne baada ya Nabii Musa tu; bali amekuja wakati ule hali ya Waislam ilipokuwa kama hali ya Mayahudi wakati wa kutumwa kwake Isa bin Mariamu; na yule aliyeahidiwa kufika kwake katika siku hizi za mwisho ni mimi. Mungu hufanya Apendavyo. Ni mpumbavu anayepigana na Mungu, na ni mjinga anayeleta hoja na kusema mbele yake; "Siyo hivi bali inafaa hivi". Na Mwenyezi Mungu Amenituma pamoja na ishara zenye kung'aa zaidi ya elfu kumi. Na moja yao pia ni Tauni. Basi anayefungamana na mimi ki kweli kweli, na anakuwa mfuasi wangu kwa nia safi na kujiweka katika kunitii kwa moyo wote na kujiepusha na matamanio yake yote; huyu ndiye atakayeombewa na roho yangu katika siku hizo za mabalaa.

Safina ya Nuhu

Mshairi aandika juu ya Mshairi

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Dar es Salaam

Kutoka toleo lililopita

Ni dhahiri kwamba kwa kila anayejua yupo anayejua zaidi. Nimeshindwa kuelewa mantiki ya Profesa Mulokozi kumuita Sheikh Kaluta Amri Abedi, Kaluta Amri Abedi katika kitabu chake 'Kaluta Amri Abedi Shujaa aliyesahaulika'. Ni dhahiri ya kwamba kabla hajaenda Pakistan kwenye masomo Sheikh Kaluta Amri Abedi aliitwa Mwalimu Kaluta Amri Abedi. Sheikh ina maana mbili katika kiarabu. Mzee, na mtaalamu wa dini ya Kiislam. Mtu aliyefanya kazi ya ubalozi humfanyii ihsani unapomuita Balozi, ni haki yake. Siwezi kujisikia vizuri kumuita Balozi Jobu Lusinde, Jobu Lusinde. Lakini kama tulivyosema huenda kuna mantiki katika kufanya hivyo. Niko tayari kujifunza.

Ukisoma kwa makini tafsiri ya Qur'ani Tukufu iliyotolewa na Sheikh Mubarak Ahmad utagundua ya kwamba Sheikh Kaluta Amri Abedi alishiriki katika kutafsiri Qur'ani Tukufu katika miaka ya 1940 na siyo miaka ya 1950 kama alivyobainisha. Profesa Mulokozi kama alivyobainisha katika kitabu chake uk. 5 ni vizuri kuweka mambo haya sawa tusije tukaanguka katika shimo alimotumbukia Bwana Mitumbe la kumpata mtu anayeitwa Sheikh Amri Abedi Karume. Ni kweli anavyosema Profesa Mugyabusuo Mulokozi kwenye uk. 5 wa kitabu chake, makaburi ya Sheikh Mathias Mnyampala na Sheikh Shaabani Robert hayaonekani vizuri na yamefunikwa bila kuwa na matunzo yoyote. Alipozikwa Sheikh Shaabani Robert panaweza kuuzwa kwa wakati wowote. Jumuiyya ya Ahmadiyya kwa upande mwingine imetunza vizuri makaburi ya Wanajamaat ambayo yapo Wailes –Temeke katika eneo hilo chini ya mwembe lipo kaburi la Sheikh Kaluta Amri Abedi ambalo linaendelea kutembelewa na watu wengi mashuhuri kutoka ndani na nje ya nchi.

Kwenye uk. 5 kuna taarifa; 'Baadae alikuwa mjumbe wa baraza la madiwani na hatimaye kuwa meya wa kwanza wa jiji la Dar es salaam mara tu baada ya uhuru'. Tunadhani ni sahihi kusema alikuwa meya kabla ya uhuru. Uhuru tumeupata tarehe 09/12/1961 na yeye alikuwa meya mwaka 1960.

Ni dhahiri pia ya kwamba alishiriki katika kufasiri Qur'ani Tukufu kwa Kiswahili mwanzoni mwa miaka ya 1950. Inawezekana si kweli sana, wakati akiwa shuleni Tabora miaka ya 1930 Sheikh Kaluta Amri Abedi alianza kusaidia katika kufasiri Qur'ani Tukufu katika Kiswahili. Mchango wake ulikuwa hususan upande wa Kiswahili. Sheikh Mubaraka Ahmad alianza kazi ya kufasiri Qur'ani Tukufu tarehe 15 Novemba 1936 na 1937 Sheikh Kaluta Amri Abedi ndipo alipoanza shughuli za kusaidia katika kufasiri Qur'ani Tukufu. Kazi ilikwenda vizuri na 1943 muswada ulipelekwa idara ya lugha nayo idara ya lugha ilipeleka muswada kwa wataalam na wasomaji. Mwaka 1944 April yalipatikana maoni ya wasomaji na wataalamu na chapa ya kwanza ilichapishwa mwaka 1953 huko Nairobi – Kenya.

Wakati "*Mabepari wa Venisi*" kimetoka Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa amekwishafariki. Hivyo kauli ya Profesa Mugyabuso Mulokozi kuwa Sheikh Kaluta Amri Abedi alishiriki pia katika mjadala kuhusu tungo za Mwalimu Nyerere za tafsiri ya William Shakespeare ambazo zilipingwa na baadhi ya wanazuoni kama vile Rydin Haris kwamba hayo hayakuwa mashairi ya Kiswahili inahitaji maelezo kidogo. Sheikh Kaluta Amri Abedi alipewa na Mwalimu J. K. Nyerere ili atizame tafsiri yake ya *Julius Kaisari* naye Sheikh Kaluta Amri Abedi alitoa ushauri ambao Nyerere aliuita ushauri wa kibingwa.

Tukio lolote kama halina somo ndani yake uzito wake unapungua kwa kiwango kikubwa. Uhusiano wa washairi hawa mahiri una funzo gani kwetu? Magwiji hawa wawili walithamini sana lugha ya Kiswahili. Mapenzi yao yaliwapelekea kuandika vitabu na kujishughulisha katika harakati za kukuza Kiswahili. Mapenzi hayo yanaonekana kupungua kwa hivi sasa. Ni wajibu wetu na sisi kuiga mwenendo wao ili kukuza lugha hii ambayo ni zawadi ya thamani kutoka kwa Allah.

Upo ushahidi wa dhahiri unaonesha mafanikio bora ya malezi. Malezi yaliyojengeka kwenye mapenzi. Sheikh Amri aliwapenda sana watoto wake. Licha ya kuwa na shughuli nyingi alipata fursa ya kuzungumza nao. Siku moja aliwapa vitabu vya dini katika Kiswahili ili wavisome na wote hawakuweza kusoma Kiswahili. Asubuhi yake aliwahamisha kutoka shule ya Aghakhani ya Kiingereza na kuwapeleka shule ya Mnazi Mmoja iliyokuwa inafundisha Kiswahili. Hapo tunamaizi ghera ya dini ya Lugha ya Kiswahili. Malezi hayo yamezaa matunda



Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwa kwenye moja ya mikutano ya chama cha Washairi

yanayoonesha mapenzi ya watoto kwa baba na lugha ya Kiswahili. Kitabu cha '*Almasi ya Afrika*' ni kumbukumbu ya maisha ya sheikh Amri kilichoandikwa na mwanae Sheikh Bakri Amri Abedi kati ya watoto wa Sheikh Amri wawili wamejitokeza kuwa watunzi wazuri wa mashairi ingawaje hawakuandika sana. Suheil Kaluta aliandika mashairi ingawaje sio mengi naye Amir Kaluta ametunga mashairi na moja ya shairi lake maarufu ni 'Panya'.

Bwana Mathias E. Mnyampala nae aliwapenda wanae na kuwapa malezi mema. Utunzaji wa maandishi ya Mnyampala kama ulivyofanywa na mwanae Charles ni alama ya mapenzi na kuthamini kazi ya baba yake. Hapana shaka 'ukiona vyaelea vimeundwa'. Malezi mazuri ndio yametupatia vijana amabao kwa kiwango wameendelea katika ustawishaji wa lugha ya Kiswahili. Kuna haja ya kuwalea watoto wetu kwa mapenzi ili hatimaye waendelee vile vitu ambavyo sisi tunavithamini.

Mapenzi kwa Kiswahili kwa watunzi hawa hayakuishia kwenye maneno tu. Mapenzi hayo yalitafsiriwa kwa vitendo. Kwa juhudi kubwa Sheikh Kaluta Amri Abedi mwaka 1959 alishiriki katika kuitisha mkutano wa watunzi wa mashairi ya Kiswahli uliofanyika katika ukumbi wa Ahmadiyya uliyopo katika msikiti wa Masjid Salaam alipokuwa anaishi Sheikh Amri. Mkutano huo ulipitisha maazimio ya kuendeleza sanaa ya ushairi. Washairi wote maarufu walihudhuria isipokuwa Sheikh Shaabani Robert ambaye alikuwa amempeleka mwanae shuleni kule Uganda. Mathias Mnyampala alikisifu chama hicho na kuimba;

Chama nakifunga kamba, kamba inakishiwe
Chama natia uvumba, ubani kifukiziwe
Chama tusije kuyumba, kisha kisahauliwe
Chama na kibarikiwe, kustawi na kupendwa

Mwaka 1965 UKUTA kilipoanzishwa Bw. Mathias Mnyampala alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho na alifanya kazi nzuri ya kuendeleza sanaa ya ushairi na lugha kwa ujumla. Mapenzi yetu kwa kitu yasiishie katika maneno bali yaoneshwe kwa vitendo kama washairi wetu hawa wawili walivyoonyesha mapenzi yao kwa lugha ya Kiswahili.

Ujenzi wa Kiswahili kwa hakika ni ujenzi wa taifa na mapenzi kwa taifa. Washairi hawa wawili walionesha mapenzi yao makubwa kwa taifa letu. Sheikh Kaluta Amri Abedi alishiriki katika mapambano ya uhuru. Mwaka 1950 alikuwa Katibu wa Tanganyika African Association (TAA), umoja ambao ulizaa TANU chama cha ukombozi. Mwaka 1957 akiwa pamoja na Rashidi Mfaume Kawawa, Nsilo Swai na Oscar Salathiel Kambona Sheikh Kaluta Amri Abedi aliwakilisha TANU katika mkutano wa Tunisia uliozungumzia ukombozi wa Afika. Mwaka huo huo aliongoza ujumbe wa wazee wa TANU ili kukutana na ujumbe wa umoja wa mataifa ili kuwaeleza juu ya madhila wanayoyapata Waafrika katika nchi yao. Alitunga na mashahiri mengi yanayowahamasisha watu katika kupigania haki yao. Mathias Mnyampala kwa upande mwingine alishiriki katika harakati za ukombozi katika tawi la TAA lililokuwa chini ya yule mpiganaji mashuhuri ambaye ni Ahmadiyya Hassan Suleiman Toufiq. Mathias Mnyampala alielewa kuwa uhuru wa bendera na mizinga 21 haukuwa uhuru hasa bila ya kumiliki wenyewe njia kuu za uchumi. Hivyo mchango wake mkubwa ni alipotumia sanaa ya ushairi katika kuhamasisha wananchi katika ujenzi wa ujamaa.

Mwaka 1960 Sheikh Kaluta Amri Abedi alichaguliwa kuwa Mbunge wa Kigoma, mchango wake unajitokeza katika taarifa za Bunge (Hansard) ukizipitia taarifa hizo utaona alivyoshiriki katika kuwasaidia ndugu zetu waliokuwa katika makucha ya ukoloni. Lipo wazo pia la kuanzisha jeshi la kulinda heshima ya Afrika. Kwa mara ya kwanza na ushahidi utaupata katika Hansard katika miaka ya 1960 Sheikh Kaluta Amri Abedi alitoa wazo la kuanzisha jeshi la kujenga taifa. Sheikh Kaluta Amri Abedi alitoa wazo hili ili tuweze kuwapata vijana wenye mapenzi na nchi yao na ambao wako tayari kutetea taifa lao na kuwafanya kuwa wakakamavu.

Hao ndio watetezi wetu wa lugha ya Kiswahili. Taifa hili lina wajibu mkubwa la kuwapa nafasi inayostahili katika historia ya nchi hii. Na ikumbukwe ya kwamba kuwaenzi waandishi hao sio ihsani, bali ni haki yao tazama Uingereza wanavyowaheshimu waandishi wake. Tizama watu wanavyotembelea alikozaliwa William Shakespeare, Thomas Hardy, Charles Dicken, Emily Bronte, Jane Austen n.k. Nenda Ufaransa uone kumbukumbu ya Victor Hugo, Urusi wanamuenzi Tolstoy, Wajerumani huwaambii lolote kuhusu Goethe, mhindi atakuonyesha jino la mwisho ukimtajia Tagore, Mpakistan hutazungumza nae muda mrefu kabla hajamtaja Mohammad Iqbal, Walt Whiteman ni sauti ya roho ya yote yanayoenziwa na Wamerakani. Unawezaje kumtaja Chinua Achebe bila kuitaja nchi yake ya Nigeria?

Naisubiri kwa hamu siku rais wangu atakapokuwa nahutubia mkutano wa kimataifa na akamnukuu Shaaban Robert, Mathias Mnyampala nitaongezeka nchi moja nikimsikia mbunge wangu anaghani beti za mmoja wa washairi wetu. Je taifa haliwezi kuwa na siku maalum ya kuwakumbuka waandishi wetu? Tukafanya maonesho ya vitabu vyao? Tukafanya majadiliano juu ya fikra zao? Wakati tunakimbilia nje kutafuta misaada huenda ikawa misaada ya maana inapatikana katika maandiko ya waandishi wetu.

Moja ya mafanikio makubwa ya ukoloni ni kutufanya tudharau vitu vyetu, utu wetu na heshima yetu. Vita yetu ya pili haitaongozwa na wanasiasa bali waandishi. Tuwape fursa ili wakamilishe ukombozi wetu. Ingawa tumeonesha mchango wa mabingwa hawa taifa letu halioneshi dalili zozote za kuwakumbuka na kuwaenzi. Itakuwa ni jambo jema kama tutaweza kuwakumbuka na kuwaenzi kwani wanawakilisha utu wetu.

Masjid Salaam, Shaaban Gonga na Maendeleo ya Kiswahili Tanzania

Na Mahmood Hamsin Mubiru
Dar es Salaam



Masjid Salaam, Dar es Salaam: Makao Makuu ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania

Kutoka toleo lililopita

Shaabani Gonga alivutiwa sana kwa kuona hapakuwepo mabadiliko ya tabia kutokana na Sheikh Kaluta Amri Abedi kupanda vyeo. Na Shaaban Gonga alikuwa na mchango mkubwa katika safari ya kisiasa ya Sheikh Kaluta Amri Abedi. Itakumbukwa ya kwamba kwenye kikao kimoja cha kuteua madiwani huko Kariakoo Shaabani Gonga alipendekeza jina la Sheikh Kaluta ili agombee udiwani wa Kariakoo. Katika kikao hicho mwana Dar es salaam huyo alijenga hoja ya kumchagua sheikh Kaluta Amri Abedi. Hata hivyo wazo hilo lilizua tafrani na sintofahamu katika kikao hicho. Wajumbe walimtazama kwa jicho la chuki na dharau Shaaban Gonga. Wajumbe kwa sauti moja walisema katu hatuwezi kumchagua Kadiani atuongoze. Shabaan Gonga hakuweka neno isipokuwa kwa haraka ilimjia mara moja wazo ya kwamba alikuwa amefanya kosa. Hivyo akafikiri mbinu nyingine ili wakati wa kikao kijacho aweze kujenga hoja mpya. Mbinu aliyoitumia ni kumtembelea mjumbe mmoja mmoja nyumbani kwake na kila mjumbe aliyekutana naye alimuambia; "Ni kweli mzee wangu unanipenda mimi niwe diwani, lakini kumbuka dunia yetu imebadilika sana.
Anatakiwa mtu anayejua Kiingereza na ambaye hatimaye atawaambia umuhimu wa kutumia Kiswahili. Imani ya mtu huyu inatuhusu nini? Julius K. Nyerere ni Mkatoliki. Tunachotafuta sio kiongozi wa dini, bali atakaye tutumikia. Sheikh Amri Abedi mnamfahamu, yeye ndiye aliyeongoza ujumbe wa wazee wa TANU kukutana na ujumbe wa Umoja wa Mataifa, ametafsiri hotuba ya Mwalimu J. K. Nyerere kwa Kiswahili aliyoitoa katika Umoja wa Mataifa, hotuba inayoitwa '*Kilio cha Uhuru*'. Huyu bwana anatufaa".

Kikao cha pili kilipofanyika kazi ilikuwa rahisi sana. Kwa kauli moja alichaguliwa Sheikh Kaluta Amri Abedi mzaliwa wa Ujiji na akafanikiwa kuwa diwani wa Ilala. Na huu ndio ulikuwa mwanzo wa utumishi wa kisiasa ambao ulimfikisha kwenye cheo cha Meya wa kwanza Mwafrika wa Dar es salaam, Mbunge wa Kigoma, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Waziri wa Sheria na Waziri wa maendeleo ya jamii na utamaduni hadi alipofariki tarehe 09/10/1964.
Licha ya vyeo hivyo alivyovipata Sheikh Kaluta Amri Abedi Shaabani Gonga aliendelea kukutana na kuzungumza naye mambo yanayohusu maendeleo ya Kiswahili kwa ujumla.
Hata ulipotokea mkasa wa shairi la 'Raha' lililofanya baadhi ya washairi kufikiri ya kwamba shairi hilo lilikuwa linamhusu mtu fulani. Wazo hilo lilikataliwa na Sheikh Kaluta Amri Abedi.
Wanazuoni shairi, hizi wako nazo radhi
Ni tungo za umahiri, tutoleazo waadhi
Si zumo lilodhihiri, kuwa lengo na gharadhi
Mambo hayo tunahodhi, katika kila johari

Shaabani Gonga na Sheikh Amri walizungumza sana juu ya shairi hili, hadi Sheikh Amri alimuuza Shaaban; "Vipi Shaabani mbona umekuwa kimya katika mtanange huu?. Kumbuka kimya kina mshindo. Shaabani Gonga alitabasamu na kusema; "Sheikh mimi kuendelea kung'ang'ania jambo hili ni sawasawa kabisa kumimina petroli juu ya nyumba ambayo inaungua".

Nyumba ya Shaabani Gonga na Masjid Salaam sehemu hizi mbili ziligeuka kuwa ngome madhubuti za kulinda na kutetea lugha ya Kiswahili. Nyumba ya Shaabani Gonga ilikuwa ni nyumba ya washairi. Upo utani usemao; 'Mshairi ambaye hajawahi kubisha hodi, kulala au kupata kikombe cha kahawa nyumbani kwa Shaabani Gonga basi huyo amepoteza sifa ya kuwa mshairi safi'. Hiyo inaonesha mapenzi ya Shaabani Gonga kwa ushairi.
Naye Sheikh Kaluta Amri Abedi nyumbani kwa Shaabani Gonga kulikuwa kwake. Na Washairi wengine ni pamoja na Pala Mlanzi Hassani, Sihiyana Swaleh Mandevu (Mtenda mema), P/ Shindikiza, Hamisi Sultani Wamwera, Maliki Abdallah Mbungiro (Watachoka), Khamisi Amani Khamisi (Nyamaume), Mahmood Hamduni (Jitu kali), Mathiasi Mnyampala (Penda chako), Mohammed Ally, Makarani na Shaabani Robert kwa kuwataja wachache. Kwa hakika Shaabani Gonga amejichumia sifa ya kuwa kiungo muhimu cha Washairi wa Kiswahili, na kwa vyovyote historia ya Ushairi nchini Tanzania haiwezi kukamilika bila kupata fursa ya kuzungumza au kupata mchango wake katika kuendeleza Kiswahili. Ni kwa kukutana mara kwa mara nyumbani kwake Shaabani Gonga ndipo lilipozaliwa wazo la kuwa na chama cha Washairi.

Wazo la kuwa na chama cha Washairi lilikuwepo kwa muda mrefu na kama tutakavyoona Shaabani Robert pamoja na Saadani Abdul Kandoro walikuwa na wazo hili miaka mingi. Ni kweli katika kila tukio panatokea sababu ya kusaidia swala mlilokuwa nalo muda mrefu na hadi kupata ufumbuzi unaofaa. Inasemekana ya kwamba washairi walifanya kazi nzuri ya kutunga mashairi kufuatia ujio wa Princes Margareth. Binti huyo wa Mfalme alitungiwa mashairi mazuri na ya kuvutia yaliyomuacha na furaha tele. Yule binti aliporudi kwao akamwandikia barua Gavana wa wakati ule Sir Richard Turnbull kumshukuru kwa mapokezi na hususan kwa mashairi mazuri ya kumkaribisha.

Jambo hilo kwa Gavana kupokea barua ya pongezi na hasa kutaja furaha iliyotokana na mashairi halikuwa jambo dogo hata kidogo. Gavana alifurahi sana na akamaizi umuhimu wa kuendeleza sanaa hii. Labda si vizuri kuwa wachoyo wa fadhila, wazungu wamefanya kazi kubwa ya kuendeleza lugha ya Kiswahili. Wamefanya utafiti na kuhifadhi nyaraka nyingi za Kiswahili. Utungaji wa Kamusi, chuo cha kwanza duniani kufundisha Kiswahili huko Ujerumani, kazi nzuri ya Sir Donald Cameroon aliyekuwa Gavana wa Tanganyika na wazungu wengine waliofanya kazi nzuri ya kukilinda Kiswahili ni pamoja na Alern, Whiterey, Ridon Harriss, Knippert kwa kuwataja wachache.

Gavana Richard Turnbull alipata wazo la kuzungumza na baadhi ya waandishi maarufu wa siku hizo akiwahimiza kuanzisha umoja wao. Mmoja wapo akiwa Bw. Salum Kombo – Mwandishi wa kitabu 'Ustaarabu wa Mwafrika'. Waandishi hao katika mkutano wao aliwaeleza thamani ya mashairi ambayo walikuwa tayari wanaifahamu na akawaeleza juu ya umuhimu wa kuwa na chama cha Washairi. Kama tulivyosema awali wazo la kuwa na chama cha Washairi alikuwa nalo miaka mingi Shaaban Robert na Saadan Abdul Kandoro mwaka 1945 alieleza wazo hilo la kuwa na chama cha Ushairi. Katika ubeti huo anasema;
Watungaji mashairi, naeleza haki yetu
Natoa langu shauri, lipenye akili zetu
Mimi nimetafakari, tukifanye chama chetu
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Tukingoja kusubiri, kutendewa kazi zetu
Ni kama twajihasiri, kuzuia mwendo wetu
Tukutane tufikiri, tufanye gazeti letu
Tukifanye chama chetu, watungaji mashairi.

Nyumbani kwa Shaabani Gonga wazo hilo la chama lilijadiliwa kwa mapana na marefu. Wazo lilionekana linafaa sana. Mipango ilifanywa ya kutayarisha mkutano na kutoa mialiko kwa washairi. Kazi hiyo ya utayarishaji na kuhakikisha mkutano unakwenda vizuri alipewa Sheikh Kaluta Amri Abedi. Mpenzi huyo wa Kiswahili alifanya kazi nzuri na Washairi wafuatao walihudhuria katika mkutano huo uliofanyika katika ukumbi wa 'Masjid Salaam' – Dar es salaam. Hao ni pamoja na *Sheikh M. K. Mkono Mbera, Sheikh D. H. Mashetani, Saidi Serikali, Sheikh H. S. Palamlanzi, Sheikh K. Amri Abedi, Mathias Mnyampala, K. Mohammed Ramadhani (Chipukizi), Mahmood Hamduni (Jitukali) S. M Kombo, Suleimani Kabunji, Hamisi Amani Hamisi Nyamaume, Athumani Khalfani, M. H. Tojali (Ubaya kwao), Saidi Athumani Makarani.*

Bila shaka moyo wa kupenda Kiswahili utadunda usipoliona jina la Shaaban Robert katika orodha ya watu hao waliohudhuria.
Wakati nazungumza na Shaabani Gonga nami nilipata tabu sana na sikujizuia kumuuliza; vipi Shaaban Robert hakuweza kuhudhuria katika kikao hicho? Shaabani hakujibu aliingia ndani na kunikabidhi barua iliyoandikwa na Shaaban Robert kuhusu mkutano huo muhimu wa Washairi. Sehemu inayohusika inasema; "Nilikuwa na nia kubwa ya kuhudhuria katika hadhara yenu. Kama ujuavyo nimefanya kazi nyingi kwa kusudi ya chama hiki, lakini kwa bahati mbaya nilitokewa na kadha iliyonichukua Uganda kumchukua mtoto wangu anayesoma huko katika skuli ya Kinder Garteni (Watoto wadogo). Niliporudi nimekuta barua yako nikaona mliyoyatengeneza mazuri sana".

Mkutano huo muhimu katika maendeleo ya lugha ya Kiswahili ulifanyika katika ukumbi wa Masjid Salaam kwenye Msikiti wa Ahmadiyya uliyopo jijini Dar es salaam. Ikumbukwe ya kwamba Msikiti huo ulifunguliwa rasmi mwaka 1957 ukiwa na sehemu mbili sehemu ya Msikiti na nyumba ya Mbashiri pamoja na ukumbi mkubwa ambapo palikuwa na Ofisi na Maktaba ya kusomea vitabu. Ni dhahiri ya kwamba katika miaka ya 50 kumbi hazikuwa nyingi na hata hivyo zingelihitaji gharama. Aliyekuwa Mbashiri wa Jamaat wa Dar es salaam kwa wakati huo Sheikh Kaluta Amri Abedi aliomba ruhusa kwa Mbashiri Mkuu wa Jumuiyya Sheikh Mubarak Ahmad ili mkutano huo ufanyike katika ukumbi wa Ahmadiyya. Ruhusa ilitolewa na mkutano ukafanyika na Sheikh Kaluta Amri Abedi akiwa mwenyeji wa Mkutano huo. Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa anajulikana kwa washairi wengine kutokana na kitabu chake; "*Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri*" kilichochapishwa na East African Literature Bureau mwaka 1952.

Endelea uk. 7

Bustani ya Washairi

MUOMBENI YAKARIN - MUSIWEZE KUPOTEA

1. Bismillahi Rahmani, shairi ninaanzia
Ninaanzia shuleni, Kitonga Ahmadiyya
Ukumbusho fahamuni, kichwani kujiwekea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

2. Wazazi tufurahani, yetu shule jipatia
Maombi tangu zamani, hadi sisi twafikia
Twamshukuru manani, ombi kulipokelea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

3. Ziendee shukrani, kwa wote ziwafikie
Waliopo kamatini, na Baraka ziwakae
Waliyawaza vichwani, ni wapi shule ikae
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

4. Twashukuru wahisani, kwa ujenzi kuchangia
Hadi mwenye ishirini, kweli alijitolea
Ikafika ukingoni, ndipo ilipoanzia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

5. Sasa nawaambieni, elimu sio mzaha
Kwa kweli jitahidini, sisi tuzidi furaha
Musiishie njiani, mutatugea karaha
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

6. Wazazi wawaleteni, ada wanajitolea
Wanajinyima maini, mupate kuendelea
Mukimfata shetani, majuto mutawagea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

7. Sala zisiwapiteni, za faradhi na za suna
Tahajudi amkeni, siache kwa kusinzia
Michango jitoleeni, Mola atawajalia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

8. Wanangu angalieni, simu acha zapotoa
Sio kitu cha thamani, mfukoni jiwekea
Itakuvunja Imani, sipate kujinasua
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

9. Kama ipo mfukoni, siyo muda kutumia
Toa memoli laini, sio vitu vya sawia
Takupeleka shimoni, sipate kukuokoa
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

10. Elimu zingatieni, zuri tajifaidia
Na walimu watiini, elimu jichukulia
Na dini isiwe chini, mema mutajizolea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

11. Wazazi wapo shuleni, wavulana naanzia
Tupia macho jikoni, tamkuta wa kulea
Ni mzazi yu makini, ya kheri takumegea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

12. Akina dada bwenini, yupo wa kujivunia
Nikianza malezini, matroni anawalea
Kimfata kwa makini, kweli hamtopotea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

13. Wana wote wa shuleni, mukae mukitambua
Tayekuwa kiburini, hayupo kwenye jamaa
Atakuwa mashakani, tamzonga ya dunia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

14. Kiburi kiepukeni, Mungu Anakichukia
Kimfata firauni, peponi hutoingia
Utakuwa hasarani, mauti kikufikia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

15. Angalia kwa undani, mupate kujielewa
Mazingira ya shuleni, walimu wanavyolea
Jitahidi kwa makini, kuishika yao nia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

16. Duara pana shuleni, kila kitu angalia
Ya uzuri jifunzeni, yasiwakae mabaya
Mola wenu muombeni, mabaya kuondolea
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

17. Karamu naweka chini, hapa ninamalizia
Maombi yadumisheni, muielekee njia
Njia bora ya Manani, ndio twaisujudia
Muombeni yakarini, musiweze kupotea

Rehema Fadhili
Kitonga – Dar es salaam

USIKIDHARAU CHAKO

1. Leo chereko chereko, nimefika mtu chake
Dunia ina vituko, mambo ya upekepeke
Kila badhi uendako, kijicho budi waweke
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

2. Mtu ukipende chako, japo punje kitukuke
Ukiona cha mwenzako, kiache usikishike
Utapata masumbuko, simangizi zikufike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

3. Cha mwenzako kina mwako, methali ithibitike
Ingawa cha ndugu yako, nasaba moja na yake
Atazua machafuko, wala usikadirike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

4. Sipende mteremko, na kupanda ukumbuke
Cha bure ni choko choko, masumbufu yakufike
Mara fimbo kokokoko, ngomeni ukafungike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

5. Budi hasara iweko, mtu mdharau chake
Jeta riziki kitako, watamwita jina lake
Mpenda bure leo yuko, vijichenga vifunike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

6. Si dhabuni kitu chako, lau gwanda lipasuke
Heshimu wazazi wako, japo macho wapofuke
Penda kwenu utokako, liwe pango lisifike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

7. Uwajali ndugu zako, kila shida uwazike
Kwao kifike kicheko, ukoo uneemeke
Chema huwa kwa mwenzako, nafsi isisituke
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

8. Uipende kazi yako, ulegevu ukutoke
Mkiri tajiri yako, utumwapo utumike
Ulitenge kasiriko, maturuba uyashike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

9. Upate mradi wako, na wewe usitirike
Litukuke jina lako, na ndipo uheshimike
Kipenda kitu si chako, budi udharaurike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

10. Wapende watoto wako, kadhalika wako mke
Hadhari kauli yako, ovu usilitamke
Tumia akili zako, ndipo jambo litendeke
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

11. Shairi ni muitiko, na viziwi liwafike
Sihasimu dini yako, kwa dhamiri uishike
Tubia kwa Molla wako, maasi uyaepuke
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

12. Mtu chake mtu kwako, alalae azinduke
Likweze kabila lako, japo lugha ipotoke
Lazidi mmemeseko, lile tunda nuru yake
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

13. Wengi wana huzuniko, pindi dhiki imfike
Hapa petu poni zipo, kaue ukaokoke
Wanapata masumbuko, kwapani wazifutike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

14. Nafupisha muandiko, kitabu nikifunike
Magomeni ningaliko, maarufu pasifike
Atoleta mchafuko, tunaomba siandike
Mtu chake mtu kwao, ndiyo raha duniani.

S. W. MOHAMMED SULEIMAN (MTU CHAKE SPEAKING) – MAGOMENI

NASIKITIKA NA DOWA

1. Nasikitika na dowa, limehalibu shati
Natamani kulitowa, lakini wapi sipati
Kasha nafuwa na dawa, na bado halitakati
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

2. Shati hili nalipenda, kuvaa kila wakati
Sasa dowa limeganda, si pembeni katikati
Nalia nauma chanda, na kufumbata magati
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

3. Lingetatuka mkono, ningefanya mashaliti
Ukosefu wa sindano, ningefunga hata nati
Ingawa si mapatano, nguo kufunga boliti
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

4. Dowa hilo kubwa mno, upana kama chapatti
Ndipo najiuma meno, naona nitashititi
Isiwe ni mapatano, ya dobi kunisaliti
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

5. Kusema siyo vioja, na sema wazi siteti
Shati langu mie moja, ni ukosefu wa senti
Laukama lingechuja, ningelivaa nakoti
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

6. Hapa mwisho na simama, na weka kaditamati
Ingawa kuna lawama, kwa kuzihasim beti
Uzee una nakama, mfano wa mahututi
Nasikitika na shati, limeng'ang'ania dowa

Sihiyana Swalehe Mandevu (Mtenda mema)

KIRUKA NJIA SIOWE – KAMWE SIOLEWE NAYE

1. Nazungumza na weye, unayetaka uowe
Pamwe na weye ambaye, unapenda uolewe
Jilisini niwambiye, m iiko yake mjuwe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

2. Jilisini niwambiye, kwenye hili myajuwe
Kwayo yawasaidiye, matatani msitiwe
Naomba mnifatiye, karibuni hapa tuwe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

3. Kiruka njia mwambaye, si mume si mke awe
Hafai usiwe naye, kamwe asikumbatiwe
Haimarishi ndowaye, ni kinofu cha nguruwe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

4. Kuowana kwetu siye, libasi na uzuriwe
Bwana apate bibiye, na binti aolewe
Kasha nyote mtuliye, kwenye ibada mpowe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

5. Na ibada kwenu nyiye, ni swala na menginewe
Mitango msiatiye, mali zenu mzitowe
Wala msilimatiye, toweni msitukiwe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

6. Hivyo uolewe naye, bwana wa Imani nawe
Nawe uowe ambaye, wa mwenendo wako wewe
Mkisigana ndokiye, yeye kipanga we mwewe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

7. Kama wataka ukaye, vizuri na upumuwe
Uishi na utuliye, bila bughudha na yowe
Uyashike nikupaye, silaha ikuokowe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

8. Haya nilokupa miye, hifadhi na utukuwe
Kishapo yazingatiye, salama yako mwenyewe
Nyumba tabaki kimuye, kwa Amani na khushuwe
Kiruka njia siowe, kamwe siolewe naye

KHAMISI S. S. WAMWERA
Kimbagulile – Mbagala Rangi tatu – Dar es salaam

Masjid Salaam, Shaaban Gonga na Maendeleo ya Kiswahili Tanzania

Kutoka uk. 5

Mkutano ulikuwa wa mafanikio makubwa. Kwa siku tatu mfululizo wapenzi wa Kiswahili walijadili maendeleo ya lugha hii adhimu. Baadhi ya mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na:-

- Kuhifadhi na kustawisha sanaa ya ushairi ambayo ni urithi na maumbile ya wenyeji wa Afrika ya Mashariki.
- Ushairi kama somo linalosaidia Kiswahili
- Kuamsha bidii za watu wanaotaka kuwa washairi
- Kuwatafutia njia za kupigisha chapa kazi zote
- Kutoa mafunzo ya kukuza ustadi wa sanaa.

Hatua nyingine muhimu ya mkutano huo ilikuwa ni kuwachagua viongozi wa kuongoza chama hicho. Sheikh Mahmood Hamduni (Jitukali) wa Dodoma alichaguliwa kuwa Mwenyekiti, S. M. Kombo alichaguliwa kuwa Katibu, K. Mohammed Ramadhani (Chipukizi) wa Dar es salaam alichaguliwa kuwa muweka hazina. Chama pia kilichagua halmashauri maalum ya wataalamu. Wao walipewa jukumu la kuzikagua kazi za Washairi. Wana Halmashauri hao ni pamoja na Shaaban Robert wa Tanga, Mathias E. Mnyampala wa Dodoma, Saadan Abdul Kandoro wa Ujiji, Sheikh Kaluta Amri Abedi wa Dar es salaam na Sir Richard Turnbull Gavana wa siku hizo aliombwa kuwa mlezi wa chama hicho.

Kuzaliwa kwa chama hicho kulipokelewa kwa vifijo na nderemo. Kutoka Dar es salaam Athumani Saidi Makarani aliimba;

Yarabi nipe wajihi, niweze yangu kunena
Kiumbe nimefurahi, watunzi tumejuana
Chama chetu kimesihi, sharia zimeungana
Mola usiye khiyana, chama chetu tukuzie.

Chama chetu tukuzie, Mola usie khiyana
Mahaini wazuie, wasije tukawaona
Nyoyo tutakasie, tulipende letu shina
Mola usiye Khiyana, chama chetu tukuzie.

Mola m wingi wa Rehema, tujalie waungwana
Tukuzie chetu chama, kwa marefu na mapana
Tuepushie khasama, khasama haina maana
Mola usiye Khiyana, chama chetu tukuzie.

Kutoka jiji la gharama, bandari ya salama, mzawa wa jiji hili Shabani Gonga (Chuma) hakuweza kuzuia sururi yake;

Tanganyika kuna kitu, kitu gani kuna chama
Tunawaomba wenzetu, tuungane kwa salama
Tutakubaliwa watu, tutende kazi ya wema
Chama tumeishaunda, waandishi tuungane

Shirini na tatu machi, tulipokiunda chama
Na mzee wa kidachi, amekuwa mwanachama
Jina lake silifichi, wa kabunji ninasema
Chama tumeishaunda, waandishi tuungane

Mengi tumeyapitisha, yenye hadhi na heshima
Wa mwanza na wa Arusha, karibuni kwenye chama
Pemba unguja mwatosha, kuwa wote wanachama
Chama tumeishaunda, waandishi tuungane

Kutoka Dodoma Machichimi alikuja Mathiasi Mnyampala (Penda chako) huku ameshika zeze lake na akaimba;

Chama nakifunga kamba, kamba inakishiwe
Chama natia uvumba, ubani kifukiziwe
Chama tusije kuyumba, kisha kisahauliwe
Chama na kibarikiwe, kustawi na kupendwa

Chama vyema kukipenda, kipambwe kunadhifiwa
Chama kisije kuyumba, twaomba kibarikiwe
Chama Yarabi Muumba, baraka kifanikiwe
Chama tumeishaunda, waandishi tuungane

Chama kiwe kama mwamba, mapaa pia yatiwe
Chama ni nguzo ya nyumba, iliyojengwa kwa imara
Chama ndio kinaomba, Inshallah kijaaliwe



Mwalimu Nyerere na washairi wengine wakiwa Masjid Salaam, Dar es Salaam.

Ni dhahiri kama tulivyoona Masjid Salaam na nyumba ya Shaaban Gonga viligeuka kuwa sehemu muhimu katika kukuza Kiswahili. Kama vile kuku anavyowakusanya vifaranga wake. Shaabani Gonga alikuwa kiungo muhimu kwa washairi nchini. Wengi walikutana kwake na wakajuana. Lakini Shaaban Gonga alijiepusha na ile methali isemayo; "Unamtembelea asiyekutembelea kama nyoka". Yeye alijitahidi kuwatembelea rafiki zake na kutumiana zawadi na kuandikiana nao barua. Mwinyikhatibu Mohammed alikutana na Shaabani Gonga mara baada ya Mwinyihatibu Mohammed kujuana na Sheikh Kaluta Amri Abeid. Ni sheikh Amri aliyempa habari za mshairi chipukizi Hamisi Amani Hamisi Nyamaume, Mahmood Hamduni (Jitukali), Farahani Kitenge, Mathias E. Mnyampala – washairi ambao usuhuba wao na Shaaban Gonga ulikwenda hadi kufikia ile hatua Waswahili wasemayo; "Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki".

Shaabani Gonga alifunga safari hadi Dodoma kuwatembelea washairi wa huko na kwa furaha alipokelewa kwa mapokezi makubwa. Kila nyumba ya Mshairi aliitembelea. Lakini jambo moja waliloligundua washairi hao ni kwamba wakati huo Shaaban Gonga hakuwa na mke. Jambo hili halikuwafurahisha kwani ndoa kwa rijali ni jambo ambalo haliepukiki. Hivyo Hamisi Amani Hamisi Nyamaume alifanya mpango hadi Shaaban Gonga alipata mke huko Singida. Mke huyo ndiye aliyempatia binti kwa jina la Zainabu. Ndoa hiyo ilileta furaha na buraha na kusababisha uandishi wa mashairi ya "Dira" yanayoshangilia ndoa hiyo.

Lakini washairi wa Dodoma nao walikuwa wanamtembelea Shaaban Gonga. Ni katika moja ya safari hiyo ndipo Sheikh Kaluta Amri Abedi na Mathias E. Mnyampala walipoanzisha urafiki mkubwa. Washairi hao wametoa somo kubwa ya kwamba tofauti zetu za dini haziwakatazi watu kushirikiana na kusaidiana na kwamba inawezekana kabisa kutokea kuelewana na kushirikiana. Ni urafiki huo uliozaa kitabu cha 'Maisha ya Hayati Sheikh Kaluta Amri Abeid kilichoandikwa na Mathias E. Mnyampala na Sheikh Amri kuandika Dibaji katika Dibaji ya Diwani ya Mathias E. Mnyampala iitwayo "Waadhi wa Ushairi".

Kutokana na miaka mingi ya kuishi na kufanya kazi Pangani akiwa Liwali, Mathias Mnyampara alikuwa amejifunza usomaji wa Qur'ani Tukufu. Kukutana k wake na Sheikh Kaluta Amri Abedi kulikuwa kwake ni kama nyota ya jah. Kwani kwa miaka mingi alikuwa na hamu na shauku ya kujifunza mashairi ya kiarabu. Sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa na sifa ya pekee miongoni mwa washairi wa Kiswahili. Licha ya kuwa na shahada ya mambo ya dini, yeye aliyafahamu vilivyo mashairi ya Kiingereza, Kiarabu, Kiurdu na Kiajemi. Mashairi ya Kiajemi alifundishwa na Mwanachuoni na Mhubiri wa Islam Sheikh Jalaludin Qamar.

Waliokuwepo enzi hizo wanaeleza jinsi washairi hawa wawili (Sheikh Amri na Mathias Mnyampala) walivyokuwa wanajadili na kuchambua mashairi na kuziangalia kanuni za mashairi ya kiarabu. Ulikuwa ni wakati mzuri sana huo kwani waliweza kujadiliana na kubadilishana mawazo.

Kutokana na uhusiano huo ulioanzia nyumbani kwa Shaabani Gonga Mathias Mnyampala kama tulivyokwisha ona hapo juu alijenga urafiki mkubwa na Sheikh Amri waliaminiana na kuheshimiana na Mathias alikuwa akitembelea mara kwa mara Masjid Salaam alipokuwa anaishi Sheikh Kaluta Amri Abedi. Nakumbuka mwaka mmoja kabla ya kifo chake Mathias Mnyampala mwaka 1968 nilikutana nae katika ukumbi wa Masjid salaam akisoma magazeti. Mara alikuja Sheikh Muhammad Munawwar Mbashiri Mkuu na akamtolea Assalaam Alaikum na Mathias Mnyampala kwa bashasha alijibu Waleikum salaam warahmatullah wabarakaatuh. Sheikh Muhammad Munawwar alimwambia Mathias Mnyampala kuwa utenzi wake wa Injili ulikuwa umejibiwa na Mwalimu Hamisi Sultani Wamwera.

Alipokuwa amebarizi pale na kanzu yake nyeupe ya darizi na kofia ya kiua, ungefikiri umekutana na mswahili kutoka Unguja. Mathias Mnyampala aliweza kwenda sawa na mahali. Nilifurahi sana niliposoma shairi lake lililokuwa linawahimiza Waislam kufunga mwezi wa ramadhani. Tizama ukaribu aliokuwa nao na rafiki yake Sheikh Kaluta Amri Abedi. Katika shairi hilo Mathias Mnyampala anaimba;

Moyo umengia huba, tungo kutia hamamu
Dhehebu kama nasaba, dini kutenga sehemu
Bali sitaki kalaba, nataka washa sitimu
Hima hima islamu, mwezi faradhi wa toba

Habbul Izzat toba, hima hima Islamu
Hima nguzo tano haba, kamilifu zimetimu
Wa ramadhani ya toba, hutuletea naima
Hima hima islamu, mwezi faradhi wa toba

Ya faidhi na ya toba, ukapate maasuma
Siwe na imani haba, ukitubu kwa karima
Sio kula na kushiba, kwa kufuata vitamu
Hima hima islamu, mwezi faradhi wa toba

Mvuto uliomleta Mohammed Ali msikitini ni kutaka kukutana na mtunzi wa sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri. Kitabu ambacho kilimletea sifa sana Sheikh Kaluta Amri Abedi na kikashangiliwa katika ulimwengu wa Kiswahili. Mohamed Ali Al-Bukhri alikuwa ni mshairi mahiri wa Kiswahili aliyetokana na ukoo wa waandishi. Babu yake Hemedi Abdallah anakumbukwa kwa utenzi maarufu wa 'Hassan na Hussein' na 'Wadachi kutamalaki mlima'. Makala zake katika gazeti la Ngurumo ni ushahidi wa elimu yake juu ya ushairi. Sheikh Amri Abedi na Mohamed Ali walielewana vizuri kwani wote walikuwa ni mabingwa wa mashairi ya Kiarabu. Mohamed Ali alikuwa akija msikitini – Masjid Salaam mara kwa mara na hapo ndipo alipokutana na mpwawe Sheikh Amri Bw. Saadan Abdulkandoro. Uhusiano huo wa Kandoro na Mohamed Ali ndio uliopelekea Mohamed Ali kuandika shairi la kupongeza diwani ya Saadani alipoimba;

Mashairi ya Kandoro, meyasoma kwa makini
Meyasoma kwa weroro, kutuvu na tamakuni
Hutaiona kasoro, ya vina wala mizani
Tungo ni tungo hizino, alizoandika Kandoro.

Kasoro taionaje, kwa bingwa mtemedeni
Kasoro itakuwaje, kwa malenga wa zamani
Kasoro imfikeje, mtimilifu wa fani
Tungo ni tungo hizino, alizoandika Kandoro.

Urafiki wa Mohamed Ali na Sheikh Kaluta Amri Abedi ulidumishwa sana na kalamu na hamu ya washairi hao kupenda kusoma. Kila sheikh Amri alipokwenda safari zake nje ya nchi hakukosa kumletea rafiki yake Mohamed Ali Kitabu.

بسم الله الرحمن الرحيم

JALSA SALANA TANZANIA 2015

Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry anapenda kuwatangazia Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kwenye siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 02, 03 na 04 Oktoba 2015, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah.

Wanajumuiya wote wanaombwa wajitahidi ili wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo.

Aidha Masheikh, Marais na Walimu wa mikoa na matawi yote nchini wanaagizwa kujitahidi kuwahimiza wanajumuiya kuhudhuria kwenye Jalsa hiyo.

Ifuatayo ni ratiba ya Jalsa Salana mwaka huu.

KIKAO CHA KWANZA: IJUMAA JIONI - 02/10/2015		
MUDA	**TUKIO**	**MHUSIKA**
9:00 – 10:00	Kusikiliza hotuba ya Ijumaa ya Khalifa mtukufu a.t.b.a.	Wote
10:00 – 10:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na Tafsiri (59:19-25)	Sheikh Khawaja Muzaffar
10:10 – 10:20	Usomaji wa Shairi: **Kiukeni Kuta hizi .....**	Mwl. Nassoro Hussein
10:20 – 11:20	**Hotuba ya Ufunguzi wa Jalsa 2015**	Amir Sahib
11:20 – 11:50	**Hotuba ya Mgeni Maalum**	**Mgeni Maalum**
KIKAO CHA PILI: JUMAMOSI ASUBUHI - 03/10/2015		
3:30 – 3:40	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na Tafsiri (62:1-6)	Mwl. Athumani Mawingu
3:40 – 3:50	Usomaji wa Shairi: **Muhammad Muungamu**	Mwl. Muhammed Habibu
3:50 – 4:00	**Kumkaribisha Mgeni rasmi**	***Amir Sahib***
4:00 – 4:30	**Hotuba ya Mgeni Maalum**	**Mgeni Maalum**
4:30 – 5:10	**Mada 1: Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ni Dhihirisho lililo wazi la uwepo wa Allah.**	Sheikh Khawaja Muzaffar
5:10 – 5:50	**Mada 2: Mifano iliyo hai ya kukubaliwa kwa maombi ya Makhalifa wa Jamaat Ahmadiyya.**	Sheikh Asif Batti
5:50 – 6:00	Usomaji wa Shairi/Qasida	Atfalul Ahmadiyya
6:00 – 6:40	**Mada 3: Hadhi ya Imam Mahdi mbele ya macho ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. na wajibu wa kumuamini.**	Mwl. Shaban Lusseza
6:40 – 9:00	Sala ya Adhuhuri / Alasiri na mapumziko	Wote
KIKAO CHA TATU : JUMAMOSI JIONI - 03/10/2015		
9:00 – 9:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu na tafsiri (41:31-36)	Fadhluilahi M. Ame. (Ahmadiyya Sec. School.)
9:10 – 9:20	Usomaji wa Shairi: **Msaada wa Wenye Shani**	Mwl. Ashraf Ndembo
9:20 – 9:50	**Hotuba ya Mgeni Maalum**	**Mgeni Maalum**
9:50 – 10:40	***Salamu za wageni waalikwa mbalimbali***	***Wageni waalikwa***
10:40 – 11:20	**Mada 4: Mchango wa Khilafat Ahmadiyya kwa Maendeleo ya Kisiasa na Kijamii ya Afrika.**	Ali Khamis Mbambwa
11:20 – 12:00	**Mada 5: Maana na Mbinu za Ujasiriamali sawa na Mafundisho ya Islam.**	Seif Hassan Nakuchima
KIKAO CHA NNE: JUMAPILI ASUBUHI - 04/10/2015		
3:30 – 3:40	Usomaji wa Qur'ani Tukufu (16:126-129)	Mwanafunzi kutoka Jamia Ahmadiyya Morogoro.
3:40 – 3:50	Usomaji wa shairi: **Muhammad Ni Nuru**	Mwl. Makarani Balama
3:50 – 4:10	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
4:10 – 4:50	**Mada 6: Mafundisho ya Qurani Tukufu na Amani ya Dunia.**	Sheikh Bakri Abedi
4:50 – 5:30	**Mada 7: Jihadi Aliyopigana Masihi Aliyeahidiwa katika kuitetea Islam.**	Sheikh Waseem Khan
5:30 – 5:40	Usomaji wa Shairi/Qasida	Nasiratul Ahmadiyya
5:40 – 6:20	**Mada 8: Nafasi ya Ubalozi wa Islam aliyonayo kila Mwanajamaat Ahmadiyya.**	Mzee Yusuf Dadi Mmoto
6:20 – 7:00	**Mada 9: Muongozo wa Hadhrat Khalifatul Masih a.t.b.a. juu ya Mahubiri na Malezi ya Wanajumuiya Wapya.**	Abdulrahman M. Ame
7:00 – 9:00	Sala ya Adhuhuri / Alasiri na mapumziko	Wote
KIKAO CHA TANO: JUMAPILI JIONI - 04/10/2015		
9:00 – 9:10	Usomaji wa Qur'ani Tukufu (61:11-15)	Sh. Hafiz Mahmood Ahmad Tahir - Jamia
9:10 – 9:20	Usomaji wa shairi: **Mazuri hasa ya Hamu**	Mwl. Mustafa Mambo
9:20 – 9:40	***Hotuba ya Mgeni Maalum***	***Mgeni Maalum***
10:20 –	**Utoaji wa zawadi/Hotuba ya Amir Sahib/Kufunga Kikao/Maombi.**	Amir Sahib

Amir Sahib ashiriki Mkutano wa Amani Zanzibar

Na Mwandishi Wetu

Amir sahib, Jamaat Ahmadiyya Tanzania, Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alikuwa ni miongoni mwa washiriki wa Mkutano wa amani wa viongozi wa Dini wa kanda ya Afrika Mashariki.

Mkutano huo ambao uliandaliwa na Shirika la Global Peace Initiative lenye Makao yake nchini Marekani ulifanyika katika hotel ya Milea Zanzibar kuanzia tarehe 21 hadi 24 Julai mwaka huu 2015.

Mbali na kuwakutanisha viongozi wa dini na Madhehebi kadhaa Afrika Mashariki wageni wengine kutoka nchi kadhaa za Afrika, Asia na Amerika walikuwepo kwenye mkutano huo.

Aidha Marais kadhaa wastaafu wa kanda ya Afrika ya Mashariki na SADEC walihudhuria mkutano huo.

Mkutano ulikuwa ni jukwaa maridhawa la viongozi wa dini kutambuana na kubadilishana mawazo.

Amir sahib alitumia nafasi hiyo kuitambulisha Jamaat pamoja na shughuli inazozifanya hasa katika nyanja ya kutetea amani ya nchi na dunia kwa ujumla.



Picha ya pamoja ya viongozi wa dini walioshiriki mkutano wa Amani Zanzibar , ulioitishwa na Shiriki Global Peace Foundation

KUJIUNGA NA JAMIA PAMOJA NA DARASA LA HIFDH 2015

Kwa Masheikh wa Mikoa, Marais wa Mikoa, Walimu na Marais wa Matawi yote nchini:

Sawa na Agizo la Amir sahib ninapenda kuwatangazia kwamba mwaka huu mara baada ya Jalsa Salana kutakuwa na mtihani pamoja na usaili kwa wale watakaotaka kujiunga na Jamia Ahmadiyya pamoja na Darasa la Hifdh (Kuhifadhi Qur'an Tukufu).

Hivyo ninakuombeni mtilie mkazo suala hili pamoja na kutoa hotuba za kuelezea Baraka za kujitolea maisha Waqf, pamoja na kuhifadhi Qur'an kwani bado inaonekana vijana wengi hawajui maana ya Baraka za Waqfu na kuhifadhi Qur'an. Aidha vijana wanaotaka kujiunga na mpango wowote kati ya hiyo wafike kwenye Jalsa ya mwaka huu.

Yafuatayo yanafaa kuzingatiwa kwa anayetaka kujiunga na Jamia Ahmadiyya:

1. **Awe amesoma shuleni angalau hadi Form Four. Vyeti vyake vya shule aje navyo wakati wa Jalsa.**
2. **Awe na umri usiozidi miaka 20, awe hajaoa na awe na Afya nzuri.**
3. **Awe anajua kusoma Quran Tukufu (matini yake) pia awe anajua masuala madogo madogo ya kidini (deen maalumaat).**
4. **Awe anajua maana ya Waqf, awe na tabia nzuri na awe na jazba ya kuitumikia dini bila masharti yoyote.**
5. **Wakati wa usaili aje na barua ya uthibitisho wa Mbashiri wake wa mkoa pamoja na Rais wa tawi lake.**
6. **Atapewa mtihani wa kuandika pamoja na usaili na baada ya hapo ndipo itathibitishwa kupata nafasi au kukosa.**
7. **Kwa kijana ambaye amejiunga na Jumuiya miaka ya karibuni, ataweza kupata nafasi ya kujiunga na Jamia iwapo ameshakaa ndani ya Jamaat kwa angalau miaka miwili.**

Yafuatayo yanafaa kuzingatiwa kwa anayetaka kujiunga na Darasa la Hifdh:

1. **Awe anajua kusoma Quran Tukufu (matini yake). Pia awe na mapenzi na shauku ya kuhifadhi Qur'an tukufu.**
2. **Awe na umri kati ya miaka 11 hadi miaka 14.**
3. **Awe na afya nzuri, awe na tabia njema na awe na uwezo wa kuishi hosteli bila ya wazazi wake.**
4. **Wakati wa usaili aje na barua ya uthibitisho wa Mbashiri wake wa mkoa pamoja na Rais wa tawi lake.**
5. **Atapewa mtihani wa kuhifadhi sehemu ya Qur'an tukufu pamoja na usaili na baada ya hapo ndipo itathibitishwa kupata nafasi au kukosa.**

Wassalaam, Wenu.
Sheikh Abid Mahmood Bhatti,
PRINCIPAL JAMIA AHMADIYYA, MOROGORO, TANZANIA.

Shinyanga yapata Mwanga

Kutoka uk. 12

na Kikristo mkoni Shinyanga walialikwa kwenye mkutano huo.

Akitoa hotuba ambayo ilikuwa ndio kiini cha mkutano huo, Amir sahib alieleza kwamba Islam maana yake ni amani itokanayo na utii, na kwamba kiini cha dhana hiyo ni kupata amani iliyokamilika na furaha ya kudumu kutokana na kutekeleza matakwa ya Allah, Muumbaji wa ulimwengu.

Alisema duniani leo tunashuhudia hali ya kusikitisha ya migogoro mikubwa wa kidini; baina ya dini moja na nyingine na baina ya makundi ya wanadini wa dini moja. Kutokuaminiana na chuki baina ya dini moja na nyingine na hata baina ya dhehebu moja na jingine kunaonekana kuzidi kuongezeka siku hadi siku.

Akasema, hata hivyo la kusikitisha zaidi ni hili kwamba pamoja na kuwa Islam ni dini iliyokuja kujenga amani duniani, wafuasi wake wananyooshewa kidole kwamba wamekuwa chanzo cha uvunjifu wa amani katika sehemu kadhaa duniani. Hili bila shaka kwa upande fulani linachangiwa na waislamu wenyewe kutoelewa vya kutosha mafunsisho ya dini yao. Wanafanya mambo yaliyo kinyume na mafundisho ya dini yao, kama vile kuanzisha makundi ya vita kwa jina la jihadi na kujilipua na kuuwa watu wasio na hatia kwa jina la Islam. Matokeo yake wanaupaka matope Uislam na kuufanya usieleweke zaidi kwa wasio Waislamu.

Amir sahib akasema kwamba Uislamu umefundisha misingi ya amani na akaitaja kuwa:

1. Islam inatambua ukweli wa Manabii wote, inaagiza kuwamini na kuwaheshimu waanzilishi wa dini zote duniani.

Mwenyezi Mungu anasema:

Wala msiwatukane wale ambao wanawaita kinyume cha Mwenyezi Mungu wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kupita kiasi bila kujua. Hivyo Tumewapambia kila watu vitendo vyao, kisha marejeo yao yatakuwa kwa Mola wao, naye Atawaambia waliyokuwa wakitenda..... (6:109)

2. Islam inafundisha udugu wa wanadamu wote na inapinga wazo la kujiona bora kwa sababu ya rangi au kabila.

Mwenyezi Mungu anasema:

Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari. (49:14)

3. Islam inahimiza kufanya uadilifu uliokamilika hata mbele ya maadui.

Qur'ani Tukufu inatufundisha: Na uadui wa watu usiwashawishini, kwa sababu waliwazuilieni Msikiti uliotukuzwa, ya kwamba mruke mipaka. Na saidianeni katika wema na utawa, wala msisaidiane katika dhambi na uasi. Na mcheni Allah; hakika Allah ni mkali wa kuadhibu. (Sura 5: 3).

4. Islam inafundisha uhuru kamili wa kuabudu.

Mwenyezi Mungu anatuagiza: Hakuna karaha katika dini; hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu; 2:257.

Amir Jamaat alikamilisha hotuba yake kwa kuwaomba wote waliohudhuria washiriki katika juhudi hii ya kuondoa dhana potofu kuwa Islam ni dini ya kigaidi.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga pamoja na kuishukuru Jamaat Ahmadiyya kwa kuandaa mkutano huo aliisifia kwamba imeonyesha mfano unaostahili kuigwa na wengine. Akaahidi kwamba mkoa wake utafanya mkutano kama huo na kuzialika dini zote ili kubadilishana mawazo juu ya mafundisho ya amani ndani ya dini zao.

Wageni kadhaa waliofika kwenye mkutano huo walipata nafasi ya kutoa maoni yao ambapo kwa ujumla wote walisifia juhudi hizo na kuziunga mkono.



Picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa msikiti wa Masjid Masroor Jamaat ya Kidanda, Shinyanga.

Baada ya mkutano huo wa amani, mnamo Siku 30/7/2015 Amir sahib alifungua misikiti ya Shabuluba na Kidanda.

Akianzia na ufunguzi wa msikiti wa Shabulula, Amir sahib na msafara wake walifika kijijini hapo majira ya saa nne asubuhi ambapo alikata utepe kuashiria uzinduzi wa msikiti huo, ikifuatiwa na maombi ya kimya. Baadae Amir sahib aliwakumbusha ndugu wapatao 200 ambao walihudhuria uzinduzi huo kwamba Jamaat imeamua kujenga msikiti huo ili kuitikia wito wa ndugu wa kijiji hicho wa kujiunga na Ahmadiyya na hivyo ilikuwa ni wajibu wa Jamaat kuwapatia mahala pa kuabudia.

Hata hivyo Amir sahib aliwakumbusha ndugu hao kwamba baada ya Jumuiya kutimiza sehemu ya wajibu wake sasa ni juu yao nao kuonesha kuuthamini msikiti huo. Aliwakumbusha kwamba baada ya kujiunga na Jamaat Ahmadiyya jambo kubwa na la msingi kabisa wanalotakiwa kulifikia ni kubadilisha mienendo yao na kuwa ya Kiislam. Akawaonya kwamba iwapo hawatobadilika basi kujiunga kwao katika Jamaat Ahmadiyya hakutowaletea manufaa yoyote. Pia aliwataka wautumie vizuri uwepo wa mwalimu kwenye tawi lao ili waweze kujifunza mambo yote ya msingi yahusuyo ibada za kila siku ikiwemo Sala pamoja na kujifunza kusoma Quran.

Naye Mwenyekiti wa kijiji hicho Bw. Pascal Ngussa alisifia juhudi za Jumuiya na kusema kwamba sasa wamepata kituo ambacho hawakukitarajia kuwepo kijini hapo.

Baada ya ufunguzi ndugu wote wakiwemo viongozi waalikwa kutoka uongozi wa kijiji walipata chakula cha mchana.

Jioni ya siku hiyo hiyo Amir sahib na msafara wake walifika kijiji cha Kidanda ambako nako taratibu za ufunguzi zilifanyika kama ilivyokuwa kwenye Jamaat ya Shabuluba.

Amir sahib aliwakumbusha ndugu wa tawi hili kwa maneno yale yale aliyowakumbusha tawi la Shabuluba na kuwasisitizia kwamba baada ya kujiunga na Ahmadiyya wanatakiwa wawe mfano mwema ili ndugu wengine waweze kuona mabadiliko waliyoyapata na jambo hilo ndilo linaloweza kuwavuta wengine. Akawaambia kwamba duniani kuna makundi mengi ya waislamu kwa idadi ya mamilioni lakini wote ni waislamu wa majina tu sio wa matendo, na hivyo Mwenyezi Mungu amemtuma Masihi na Mahdi ili kuja kuurejesha Uislamu wa matendo katika usahihi wake. Pia aliwakumbusha kwamba sisi ni wenye bahati sana kwa kumkubali Imam huyu wa zama lakini bahati yetu itakuwa na maana tu iwapo tutabadilika na kuacha mila zetu za zamani na kufuata mafundisho ya Islam.

Siku iliyofuata ambayo ni Ijumaa 31/7/2015 ilikuwa ni makhsus kwa ajili ya ufunguzi wa msikiti wa tawi la Nsalala ambapo Amir sahib aliongoza pia sala ya Ijumaa hapo.

Kama ilivyokuwa kwa ufunguzi wa misikiti mingine Amir Jamaat alikata utepe kuashiria kufunguliwa kwa msikiti huo na kisha yakafata maombi ya kimya. Katika msikiti huu Amir Jamaat aliitumia hotuba ya Ijumaa kama sehemu ya kuwakumbusha Wanajamat hao wapya juu ya wajibu wao wa kufuata mafunzo kamili ya Islam baada ya kujiunga kwao na Ahmadiyya.

Aliwaeleza bayana kwamba kwa vile wamejiunga na Ahmadiyya - ambao ni Uislamu wa kweli basi hawana budi waachane na maovu yote ya hapo kabla. Aliwasisitizia kwamba iwapo hawatobadilika basi kujiunga kwao na Ahmadiyya hakutokuwa na maana yoyote.

Kimakhsusi Amir sahib alipinga dhana potofu ya kufikiriwa kwamba Jumuiya ni kundi la watu matajiri wanaopita kumwaga fedha hapa na pale kwa kujenga misikiti. Kinyume chake aliwakumbusha kwamba ujenzi huo wa misikiti unafanywa kama njia ya kuwalea wanajumuiya wapya ili waimarike na wao waweze kujitolea katika njia ya Mwenyezi Mungu.

Aidha katika misikiti yote Amir sahib aliahidi kupatikana vifaa vya umeme uzalishwao kwa mwanga wa jua ili waweze kusikiliza MTA ikiwa ni njia nyingine ya malezi kwa wanajumuiya wote duniani.

Baada ya uzinduzi wa msikiti wa Nsalala Amir Jamaat na msafara wake walimtembelea Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ofisi kwake kuitikia wito wake kwamba afike ofisini kwake kabla ya kuondoka.

Siku ya Jumamosi Amir Sahib alitemebelea mkoa wa Simiyu ambako kumepatikana tawi jipya na huko pia mbali ya kuwasalimia Wanajumuiya hao wapya alipata pia fursa ya kumtembelea Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mh. Erasto Mbwilo ofisini kwake.

Siku iliyofata Amir sahib alitembelea mjini Tarime ambako alifanya ufunguzi wa Msikiti wa Tarime Mjini baada ya kufanyiwa ukarabati mkubwa.

Kwa ujumla safari ya Amir sahib katika kanda hii imepata mafanikio makubwa na kuwa njia ya kuwapatia mwanga zaidi wanajamaat wa Shinyanga, wapya na wakongwe.



Picha ya pamoja mara baada ya ufunguzi wa msikiti wa Masjid Tahir Jamaat ya Shabuluba, Shinyanga.

Zingatieni malengo ya Jalsa

Kutoka uk. 12

wa mkweli kabisa Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika kushika tahadhari kubwa na kujali sana kuwahudumia wageni kwa kiwango cha hali ya juu kabisa.

Qur'an tukufu inatueleza juu ya huduma kwa wageni iliyotolewa na Hazrat Ibrahim a.s. Mara tu alipopokea wageni, baada ya kuwakaribisha kwa makaribisho ya amani, aliwatayarishia chakula. Hadhrat Lut a.s. pia naye anatajwa katika Quran jinsi alivyoshika hadhari ili wageni wake wasipate shida. Shida kwa wageni haitakiwi ichukuliwe kama kitu cha kawaida tu. Kwa hakika shida yoyote kwa mgeni inakuwa ni fedheha kwa mwenyeji wake.

Hii ndio sababu Islam inahimiza kuwaheshimu na kuwajali wageni. Sifa zilizo bora za Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. zinasimuliwa na hadhrat Khadija r.a. ziliongezeka zaidi baada ya kupokea wahyi wake wa kwanza ikiwemo sifa ya kuwajali wageni. Kuna maelfu ya mifano iliyo bora kabisa ya kuwaheshimu na kuwajali wageni aliyoionyesha Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. katika maisha yake. Pia alizifundisha sifa hizi kwa masahaba zake ambao nao walionyesha kwa matendo jinsi ya kuwaheshimu na kuwajali wageni kwa namna ambayo Mwenyezi Mungu akawa radhi nao.

Ilikuwa ni sunna ya Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. wakati apatapo wageni wengi kuwagawa miongoni mwa masahaba na wengine aliwachukua mwenyewe nyumbani kwake. Sahaba mmoja anasimulia kwamba wakati fulani alikuwa miongoni mwa wageni ambao Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. aliwachukua nyumbani kwake. Alienda na wageni hadi kwa Bibi Aisha r.a. na kumuuliza iwapo kuna hcochote cha kuwapatia hao.

Bibi Aisha r.a. akajibu kuna chakula kidogo tu ambacho alikuwa amemuwekea yeye Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. kwa ajili ya futari. Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. akamwambia akilete. Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. akaonja kidogo na kuwapatia wageni wake ambao walikula na kutosheka. Kisha akamuuliza tena bibi Aisha iwapo kuna chochote cha kunywa. Hadhrat bibi Aisha r.a. akaleta kinywaji ambacho pia Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. akakionja na kuwapatia wageni nao wakanywa hadi wakatosheka. Sababu ya kwa nini Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alikionja kwanza chakula na kinywaji kile ilikuwa ni kwa ajili ya kumuomba Mungu ili kibarikiwe na kiwatoshe wageni wake. Kuna mifano mingine mingi ya jinsi chakula kilivyobarikiwa kwa kuombewa na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w..

Baadhi ya nyakati wageni nao wanaweza kusababisha mazingira magumu kwa mwenyeji, lakini katika hili pia Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alituonyesha mifano iliyo bora kabisa ya kukabiliana na changamoto kama hizo. Wakati fulani mgeni mmoja alifika kwa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. na akapatiwa malazi lakini usiku akajisaidia kitandani ama kwa kusumbuliwa na tumbo au kwa sababu fulani ya kutaka kumuudhi Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w.. Asubuhi, badala ya kulalamika, Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alichukua shuka alizochafua yeye mwenyewe na kuanza kuzisafisha.

Kutokana na mifano hiyo ya kushangaza Masahaba zake pia nao walionyesha kujitolea kwa hali ya juu katika kuwahudumia wageni. Mfano ambao ni wa kipekee ni ule wa sahaba mmoja na mke wake waliowafanya watoto walale ili chakula kidogo ambacho kilikuwa kimeandaliwa kwa ajili yao hao watoto waweze kula wageni na wakati wa chakula wakajifanya taa imezimika na hawakuiwasha hadi wageni walipomaliza kula chakula na kutosheka wakati wao wakipapasia sahani kuonesha kwamba nao wanakula.

Asubuhi yake Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alipomuona sahaba huyu akaanza kucheka na kusema Mwenyezi Mungu amefurahishwa sana na mpango wako wa jana usiku. Mwenyezi Mungu amekuwa radhi nawe na amemfunulia Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. habari yote hiyo.

Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alisema mtu yeyote anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho basi aseme neno zuri au anyamaze. Yeyote anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho amheshimu jirani yake na Yeyote anayemuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho amkirimu mgeni wake.

Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. pia alikuwa akiwauliza wageni wamezionaje huduma walizopatiwa na wenyeji wao. Katika tukio moja wageni walisema kwamba Ee Mtume wa Allah wametuhudumia vizuri, wametupatia godoro laini la kulalia, wametupatia chakula safi na wametufunza pia juu ya kitabu na sunnah. Basi hili ndilo jukumu la mwenyeji. Watu wanaowachukua wageni wa Jalsa majumbani mwao wasitumie muda wa usiku kwa maongezi ya kawaida tu bali watumie muda huo kwa mazungumzo ya dini ili kuwapatia elimu wageni wao.

Hata katika maeneo ya Jalsa pia tunakuwa na wageni wanaotoka nje ya Jamaat. Watoa huduma katika kila makazi waoneshe tabia nzuri ili wageni wapate kuona kwamba kweli wamekuja kwenye mkutano wa kidini. Aidha wahudumu kila wapatapo muda kidogo iwe mchana au usiku, badala ya kuanza maongezi haya na yale, wajitahidi kuongea maongezi ya kidini. Jambo hili litawacha athari nzuri kwa wageni na watagundua kwamba kumbe katika siku hizi tatu Waahamdiyya wanakuwa wamejikata kabisa kutoka kwenye mambo ya kidunia.

Masahaba wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. hawakuwa wenyeji bora katika kuwapatia wageni chakula na malazi tu, bali pia kukata kiu yao ya kiroho ili warudipo makwao waweze kuwafikishia wengine pia.

Tunazo idara za Tabligh na Tarbiyyat lakini ikumbukwe kwamba kutoa lishe ya kiroho ni jukumu la kila mhudumu na linatakiwa litolewe kwa njia iliyo bora kabisa. Neno zuri na tendo jema pia ni sehemu ya dhiafat muhimu wanayotakiwa kuitoa wahudumu.

Katika zama hizi mfuasi mtiifu wa Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w., Masihi Aliyeahidiwa a.s., naye ametuonesha viwango vya juu kabisa vya kuwahudumia wageni.

Mgeni mmoja alifika Qadian baada ya kuchukua baiat na hivyo akawa na uhusiano wa kuwa Mfuasi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s., alikuwa akimkanda kanda miguu kama njia ya kuonesha heshima. wakati huo Mhindu mmoja akagonga mlango na mgeni yule akaelekea mlangoni ili kumfungulia. Lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akainuka kwa kukimbia haraka zaidi kuwahi kufungua mlango na akamwambia mgeni wewe ni mgeni na Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. ameagiza mgeni aheshimiwe, hivyo ni jukumu langu mimi kumfungulia mlango anayegonga. Hapa tunajifunza vitu viwili. Kwa upande mmoja mgeni huyu akiwa mfuasi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa akimkanda miguu lakini kwa upande mwingine kwa kujali heshima ya mgeni, Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliinuka mwenyewe kufungua mlango na kumlaki mgeni wake.

Wakati fulani mgeni mmoja pia alitembelea Qadian msimu wa baridi ili kukutana na Masihi Aliyeahidiwa a.s.. Kulikuwa na mvua na alifika usiku. Alipatiwa chakula cha usiku na akaenda kupumzika. Baadae usiku akasikia mlango ukigongwa na alipofungua akashtuka kumuona Masihi Aliyeahidiwa a.s. akiwa amekamata glasi ya maziwa yaliyo moto mkono mmoja na taa mkono mwingine. Akamwambia tulikuwa tumepata maziwa hivyo nikadhania kwamba una tabia ya kunywa maziwa usiku hivyo nimekuletea. Mgeni yule alitokwa na machozi kwa kuona jinsi Mjumbe wa Mwenyezi Mungu anavyohangaika kumuhudumia.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alikuwa na tabia pia ya kujali sana aina ya vyakula kwa wageni wake sawa na mazingira wanayotoka. Ingawaje sawa na sababu za kimipangilio wakati wa Jalsa chakula cha aina moja tu kilikuwa kikipikwa. Sasa Jumuiya kwa fadhili za Allah imepata maendeleo zaidi ya miuondo mbinu na vitu na hivyo jiko linaendelea kupika vyakula vya aina mbalimbali.

Bila shaka hakuna shida yoyote juu ya hili. Wakati mwingine baadhi ya watu bila ya sababu ya msingi hulalamika bure. Wanatakiwa wawe na uvumulivu. Ili kuwafanya waalikwa wa nje, wanaotambulika maarufu kama wageni wa Tabshir, ili wajue kile wanachokula wengine kwa jumla, basi nao wanapewa chakula cha Langar khana. Wengi wanakula kwa hamu. Nukta hapa ni kwamba utaratibu huu wa chakula maalum ulikuwa hauwezekani zamani, lakini kwa sasa unawezekana na ndio unaofanyika.

Mipango hii pia ilikuwa ikifanyika Rabwah. Kwa ujumla Waahmadiyya wote wanatakiwa wale kile kinachopikwa kwa wote, watoa huduma nao pia wale hicho hicho, isipokuwa wale wanaopewa jukumu la kuwahudumia wageni maalum, hao wale sawa na wanachowapatia wageni.

Wakati fulani zama za Masihi Aliyeahidiwa a.s., kutokana na kosa fulani la kiutendaji wageni hawakupatiwa chakula ipasavyo. Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliwasimamisha wahudumu kwa miezi 6. Pamoja na tabia yake ya upole aliyokuwa nayo, bado hakuvumilia mapungufu na unafiki katika kuwahudumia wageni. Baadae yeye mwenyewe akawa anasimamia shughuli za jikoni. Hivyo idara ya Dhiafat inatakiwa kushika hadhari sana na kuwa makini. Haitakiwi hata mgeni mmoja kuwa na manung'uniko ya aina moja au nyingine.

Dhiafat haimaanishi tu kuhudumia chakula, inamaanisha taratibu zote za jikoni, kugawa chakula uhifadhi na usambazaji wa chakula. Bila shaka kusinzia kusambaza chakula vituoni kunaweza kucheleweshe ugawaji. Dhiafat inamaanisha pia malazi ambayo yanatakiwa kuwa mazuri. Pia kuna utaratibu wa usafi, wote usafi wa jumla na wa vyoo. Sehemu za maegesho ya magari yote hayo yanamanisha dhiafat. Iwapo kutakuwa na mkanganyiko wowote kwenye hayo kunaweza kuharibu mipango ya Jalsa. Kuna kazi kubwa ya kutoa vipasha joto wakati wa baridi kali, pia kuna vigari maalum vya kuwabeba wazee na walemavu ndani ya Hadiqatul Mahdi kutoka sehemu za maegesho ya magari. Haya yote yanaangukia kwenye huduma za wageni.

Iwapo kazi hizi zitafanywa ipasavyo, basi kila kitu kitakwenda sawa. Huduma za Afya pia zinaangukia kwenye dhiafat. Kwa ufupi zaidi ya asilimia 80% ya shughuli za Jalsa zinaangukia chini ya Dhiafat - huduma kwa wageni. Kila mmoja akumbuke kwamba kutoa huduma sio jukumu la wale waliovaa beji tu zilizoandikwa 'Dhiafat', bali kila anayeshiriki kutoa huduma ya aina moja au nyingine.

Leo ni tarehe 14, August, siku ya Uhuru wa Pakistan. Kwa mnasaba huu maombi yafanywe ili Mwenyezi Mungu aijaalie Pakistan uhuru wa kweli na ailinde dhidi ya Mashekhe wenye ubinafsi. Mwenyezi Mungu aipe ufahamu jamii ya Wapakistan kuchagua viongozi wakweli na waadilifu. Mwenyezi Mungu awape ufahamu wa kuelewa kwamba uimara wa taifa umo katika kushika adili, kumpatia kila mtu haki yake na kwa kumuelekea Mungu. Ukatili unafanywa kwa Jina la Mwenyezi Mungu Aliye Mwingi wa Rehema Mwingi wa Ukarimu.

Kwa jina la Mwenyezi Mungu na Mtume Wake aliye ni Rehema kwa Waimwengu, ukatili unafanywa kila upande dhidi ya Waahmadiyya ambao wametoa mchango mkubwa na muhanga katika uundwaji na ujenzi wa taifa la Pakistan. Hivyo haijalishi mahala popote ambapo raia wa Pakistan wapo wanatakiwa wawe watii kwa taifa lao, na wamuombe Mwenyezi Mungu ailinde nchi yao. Nchi imo kwenye hatari zaidi kutokana na uadui wa ndani unaosababishwa na Mashekhe walafi na wabinafsi kuliko hata uadui wa nje. Iwapo wataiendesha nchi wakiwa na hofu ya Mungu hakuna uadui wa nje unaoweza kuidhuru nchi. Waahmadiyya wenye asili ya Pakistan wajitahidi kuomba mwisho wa jitihada zao ili Mwenyezi Mungu aifanye nchi yao yenye salama na amani.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Shwl./Dh.Qa'da 1436 AH | Agosti 2015 | Zahoor 1394 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Abdullah bin Amr bin 'As r.a. anasimulia kwamba mtu mmoja alimuuliza Mtume s.a.w.: Kitu gani bora zaidi katika Islam? Akajibu: Kuwalisha watu na kumtolea salamu yule unayemfahamu au usiyemfahamu (*Bukhari na Muslim*)

Khalifa Mtukufu awakumbusha Wanajumuiya:

Zingatieni malengo ya Jalsa

Na Mwandishi Wetu

Kwa fadhili za Mwenyezi Mungu Jalsa Salana ya Jamaat ya UK inaanza wiki ijayo. Wanaojitolea wamekuwa kwenye harakati kwa wiki kadhaa sasa huko Hadiqatul Mahdi wakiandaa mazingira kwa ajili ya Jalsa. Matayarisho haya ambayo kwa sehemu kubwa yanafanywa na Khuddam na wengine pia yamepamba moto zaidi kwenye siku 10 zilizopita. Kwa kweli si kazi rahisi kuandaa sehemu ambayo kimsingi ni shamba kukidhi kuwa mazingira ya Jalsa. Khuddam kutoka sehemu kadhaa za UK na wanaojitolea wengine wanafanya kazi kwa utaalamu wa kushangaza kabisa, na hakuna mfano wake unaoweza kuonekana duniani kote au katika taasisi yoyote. Ni rehema ya Mwenyezi Mungu kwamba ameingiza jazba hii ya kujitolea kwenye nyoyo za wale waliochukua Baiat ya Masihi Aliyeahidiwa a.s..

Iwe jua iwe mvua, vijana hawa wanajitolea bila ubinafsi kwa ajili ya Jalsa Salana iliyoanzishwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s..



Masjid Baitul Futuh London

Na katika siku za Jalsa yenyewe maelefu ya watu hujiunga nao wakijitolea ili kuwafanya wageni wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. waishi kwa utulivu na raha. Baadae muda mwingi pia huhitajika kwa ajili ya kukunja jamvi baada ya Jalsa. Hawa wanaojitolea wanakusanya watu wa rika zote, wanaume, wanawake, vijana, wavulana, wasichana na wazee pia. Hii ni jazba na subira kubwa kabisa inayooneshwa katika kuwahudumia wageni wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambayo haiwezi kuonekana nje ya jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa a.s..

Kupenda dunia na starehe zake ndio mtindo wa maisha ya leo hasa sehemu hii ya Ulaya Magharibi lakini ni katika mazingira haya haya ambayo vijana hawa wa Kiahmadiyya wanajitolea kwa unyenyekevu mkubwa na kwa namna iliyo bora kabisa. Tuwaombee hawa, ili Mwenyezi Mungu Awawezeshe kutimiza kazi zao kwa njia iliyo bora zaidi na Awalinde dhidi ya maovu yote na shida zote.

Kama ilivyo kawaida yake mara zote, Huzur a.t.b.a aliongelea somo la kuwahudumia wageni katika Ijumaa hii na akasema kwa kweli ni haja ya wakati kufanya hivyo. Hakuna shaka kwamba wengi wa wahudumu ni wazoefu na wanahudumia kwa kujituma sana lakini kuna wengine ambao ni wageni wa kutoa huduma ama ni wanajumuiya wapya au ni vijana wadogo ambao hii ndio mara yao ya kwanza kuhudumia; basi kuwakumbusha hao ni jambo la lazima. Kuwakumbusha ni jambo la lazima ili kwamba waweze kubaki na kuendeleza Sunna aliyoionyesha Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. na kutekelezwa na mfuasi

Endelea uk. 11

Shinyanga yapata Mwanga

Ziara ya Amir Sahib yaleta matumaini mapya

Na Mwandishi Wetu, Shinyanga

Amir wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmmod Chaudhry amefanya ziara yenye mafanikio makubwa katika mkoa huu wa Shinyanga.

Katika ziara hiyo Amir sahib alifuatana na Katibu mkuu wa Ziada wa Jumuiya nchini Mwl. Abdulrahman Ame, Mbashiri wa mikoa ya kanda ya Mwanza, Shinyanga na Simiyu, Sheikh Waseem Ahmad pamoja na viongozi wengine wa kanda hiyo wakiwemo Rais wa Kanda na naibu wake.

Akiwa mkoani hapa Amir Sahib alishiriki matukio kadhaa yakiwemo ufunguzi wa misikiti, mkutano wa amani mkoani Shinyanga na



Picha ya pamoja kati ya uongozi wa Jamaat Ahmadiyya pamoja na viongozi wa Serikali walioshiriki mkutano wa Amani Shinyanga. Waliokaa kutoka Kulia: Amir Jamaat Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Alli Nassoro Rufunga na Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga Mjini Bi Josephine R. Matiro,

kutembelea matawi kadhaa kuonana na wanajamaat.

Siku ya tarehe 29/7/2015 ilikuwa ni siku ya mkutano wa Amani ambao ulifanyika kwenye ukumbi wa NSSF. Mkuu wa mkoa wa Shinyanga Mh. Alli Nassoro Rufunga alikuwa ni mgeni rasmi kwenye mkutano huo. Pamoja na uwepo wa Mkuu wa mkoa viongozi kadhaa wa Mkoa huu akiwemo Mh. Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga mjini Bi Josephine R. Matiro, viongozi waandamizi wa mkoa wakijumuisha kamati yote ya ulinzi na usalama, pamoja na watendaji wengine wa kiserikali.

Aidha viongozi wa madhehebu mbali mbali ya dini ya Kiislam

Endelea uk. 10